SUPA JACKPOT
TZS. 1,062,078,169
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Papa** Benedict XVI afariki dunia, Ujerumani na UK watuma salamu

UKURASA 17

MENEJIMENTI NA WAFANYAKAZI WA **THE GUARDIAN LTD** TUNAWATAKIA WATANZANIA WOTE HERI YA MWAKA MPYA WA **2023**
The Guardian Nipashe

Nipashe
MWANGA WA JAMII
JUMAPILI
Jumapili Januari 1, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0581177
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Mamilioni yalivyookolewa kufuta Sherehe Mapinduzi

UKURASA 2



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na waandishi wa habari wa vyombo mbalimbali ikiwa ni kawaida yake ya kukutana nao kila mwisho wa mwezi. Mkutano huo ulifanyika Ikulu mjini Zanzibar, jana. **PICHA: IKULU.**

## YALIYOMO

**UKURASA WA 3**

### MURILO AONYA WANAOPENYA CHINI YA MADARAJA YA DAR

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limesema linaendelea 'kuwashughulikia' na kuwachukulia hatua za kisheria wale wote wanaopenya kwenye uzio chini ya madaraja badala ya kupita juu...

**UKURASA WA 4**

### MAMBO 14 USHIRIKIANO WA TANZANIA NA CHINA MWAKA ULIOMALIZIKA

CHINA ni taifa lenye historia ya kindugu na Tanzania, ikiwa na mzizi tangu zama miaka michache kabla uhuru wa nchi kupatikana...



## Wabambwa na mafuta ya kupikia yanayodaiwa kuwa ya wizi

UKURASA 2

# Jela miaka mitatu kwa kumpa rushwa hakimu

UKURASA 3

**MICHEZO** **SIMBA SC YAWEKA REKODI 3 LIGI BARA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA



Naibu Waziri wa Maji Meryprisca Mahundi akizungumza katika kijiji cha Mtepera wilayani Kilwa mkoa wa Lindi wakati Kamati ya Mawaziri wa Wizara za Kisekta ilipotembelea kijiji hicho juzi. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Rais Dk. Mwinyi afuta sherehe za Mapinduzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema fedha zilizotengwa kwa ajili ya sherehe za miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar zitatumika katika miradi ya elimu na sherehe hizo kwa mwaka huu hazitakuwapo.

Dk. Mwinyi alielekeza hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari Ikulu visiwani hapa na kubainisha kuwa fedha hizo ni Sh. milioni 450.

Alisema kuwa awali serikali ilipanga bajeti ya Sh. milioni 700 kwa ajili ya sherehe hizo lakini zikapunguzwa na kufikia Sh. milioni 450.

Kiongozi huyo alisema fedha hizo zilizotengwa na kuelekezwa katika elimu, hazitoshelezi kutatua changamoto zote za sekta hiyo, bali zitasaidia kupunguza baadhi ya kero zilizopo.

Alisema licha ya uamuzi wa kuzuia sherehe hizo mwaka huu, harakati za uzinduzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo zinaendelea na miradi 55 itazinduliwa na mingine kuwekewa jiwe la msingi.

Alisema miongoni mwa miradi itakayozinduliwa ni majengo ya shule, hospitali, hoteli za kitalii na baadhi ya masoko, likiwamo Soko la Darajani na masoko mengine ambayo yanaendelea kujengwa, yatawekwa jiwe la msingi.

"Sherehe hizi za miaka 59 ya Mapinduzi hazitakuwapo kama tulivyozoea kuziona zinafanyika kwenye Uwanja wa Amani na kwa sasa tunajipanga zaidi kwa sherehe za miaka 60 ya Mapinduzi ambazo zitakuwa kubwa na za aina yake zitakazofanyika mwaka 2024," alisema Dk. Mwinyi.

Akizungumzia kupanda kwa bei za bidhaa hasa vyakula, Rais Dk. Mwinyi alisema hali ya ukame na vita vya Ukraine vimesababisha kupanda kwa bei za vyakula, hasa unga wa ngano, maharage na bidhaa zingine.

Alisema Zanzibar itategemea baadhi ya vyakula kutoka Tanzania Bara, husasani maharage, mahindi, viazi, vitunguu na bidhaa zingine hivyo kutokana na ukame uliosababishwa na upungufu wa mvua, kumepelekea uzalishaji wa mazao Tanzania Bara kupungua.

"Mfano, nchi ya Ukraine ndiyo inayozalisha bidhaa ya unga wa ngano na bado vita vinaendelea nchini humo na ngano imepanda, hivyo bidhaa zinazotoka huko zitazidi kuongezeka bei," alifafanua.

Rais Dk. Mwinyi alisema Zanzibar inakabiliwa na tatizo kubwa la ufanisi mdogo wa Bandari ya Malindi kutokana na ufinyu wa bandari unaosababisha meli zinazoleta mizigo kukaa muda mrefu bandarini, hivyo kukamilika kwa ujenzi wa Bandari ya Mangapwani kutasaidia kutatua kero hiyo na wafanyabiashara kupata mizigo yao kwa wakati.

"Ukame umetuathiri, vita vya Ukraine vimetuathiri, UVIKO-19 umetuathiri, bidhaa zimepanda bei," alisema.

Kiongozi huyo alisema serikali inayo mikakati yake kukabiliana na hali hiyo, akiitaja inajumuisha kupunguza ushuru wa bidhaa ili wananchi kupata mahitaji muhimu ikiwamo chakula na kupunguza ukali wa maisha.

**HALI YA USALAMA**

Akizungumzia hali ya usalama, Rais Dk. Mwinyi alivitaka vyombo vya ulinzi na usalama kuhakikisha vinalinda usalama wa raia na mali zao bila ya kuvunja sheria.

Alisema vijana wanaofanya vitendo vya uhalifu ikiwamo uporaji wanaojulikana kwa jina la panya road, ni tatizo katika jamii, hivyo akaelekeza vyombo vya usalama lazima vihakikishe usalama wa raia pamoja na mali zao unalindwa na wahalifu wa vitendo hivyo kukamatwa na kuchukuliwa hatua stahiki.

**DAWA ZA KULEVYA**

Kuhusu dawa za kulevya, Rais Dk. Mwinyi alisema bado athari zake ni kubwa katika jamii, hivyo vita vya kuzikabili havitaisha kwa siku moja na serikali inaendelea kukabiliana na biashara hiyo.

Akiwazungumzia watuhumiwa wa dawa za kulevya walitoroka mahabusu gerezani, Rais Dk. Mwinyi alisema tayari maofisa 12 wa Jeshi la Magereza wamesimamishwa kazi kwa ajili ya uchunguzi wa tukio hilo.

"Tunaamini kuwa watuhumiwa hao wamesaidiwa kutoroka na uchunguzi ukikamilika na wataothibitika kuwa wameshiriki kuwatorosha watuhumiwa hao, hatua kali zitachukuliwa na ninampongeza Kamishna wa Magereza kwa kuwasimamisha kazi watumishi hao 12 kwa ajili ya kupisha uchunguzi," alifafanua.

# Wanaswa na shehena ya mafuta kupikia inayodaiwa kuwa ya wizi

**Na Gideon Mwakanosya, SONGEA**

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma, linawashikilia watu watano wakiwamo wafanyabiashara wawili kwa tuhuma za kukutwa na ndoo 581 za mafuta ya kupikia yanayodaiwa kuwa ni ya wizi.

Mafuta hayo yanadaiwa kuwa ni mali ya kampuni ya MO Premium Cooking Oil Limited.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Kamishna Msaidizi (ACP) Marco Chilya, aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Mwinyi Hatibu (47) ambaye ni mfanyabiashara na mkazi wa Pangani Mkoani Tanga na Adelhard Mgeni (39) mfanyabiashara wa mjini Njombe na Amos Hussein.

Chilya alisema jeshi hilo likiwa katika operesheni maalumu, lilikamata kwa awamu tofauti mafuta hayo yanayodaiwa kuwa ya wizi.

Alisema awamu ya kwanza, walimkamata Hatibu akiwa na ndoo 242 za mafuta hayo zenye ujazo wa lita 10 kila moja bila kuwa na uhalali wa kibali cha aina yoyote.

Kamanda huyo alisema baada ya mafanikio hayo, polisi kupitia idara ya upelelezi, waliendelea na upelelezi wa kina sambamba na kufanya operesheni kali na Desemba 25, mwaka jana, katika eneo la Samko walimkamata Mgeni akiwa na ndoo 399 zenye ujazo wa lita 20 kila moja mali za kampuni hiyo.

Alisema mfanyabiashara huyo alikuwa katika mpango wa kutorosha mafuta hayo baada ya kupata taarifa kuwa shehena nyingine ya bidhaa hiyo imekamatwa mikononi mwa Hatibu.

Kamanda Chilya alisema juzi kuwa upelelezi wa tukio hilo bado unaendelea na utakapokamilika watuhumiwa wote watafikishwa kwenye vyombo vya sheria kwa hatua zaidi.

Hata hivyo, Chilya alisema thamani ya mali hizo bado haijafahamika licha ya kuwa jitihada zinafanywa kuwasiliana na wahusika ili kujua thamani halisi.

Aidha, Kamanda Chilya amewaonya watu wakiwamo wafanyabiashara wenye tabia ya kufanya biashara ya magendo na kuwataka kuacha mara moja tabia ya kununua mali ovyo mtaani ambazo zinadhaniwa kuwa ni za wizi.

## HABARI KITAIFA



Mawaziri wa Wizara za Kisekta wakiongozwa na Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Dk. Angeline Mabula (wa tatu kulia) wakiondoka mkoani Ruvuma baada ya kumaliza kazi ya utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika mkoa huo juzi. **PICHA: WIZARA YA ARDHI**

# Murilo aonya wanaopenya chini ya madaraja ya Dar

**Na Halfani Chusi**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limesema linaendelea 'kuwashughulikia' na kuwachukulia hatua za kisheria wale wote wanaopenya kwenye uzio chini ya madaraja badala ya kupita juu.

Hatua hiyo imekuja ikiwa ni siku chache baada ya kusambaa kwa kipande cha video kwenye mitandao ya kijamii kikionyesha watu wakilazimisha kupenya kwenye uzio na kuvuka ng'ambo ya pili wakikwepa kutumia daraja kwenye Kituo cha Mabasi cha Magufuli kilichopo mbezi wilayani Ubungo.

Hali hiyo pia imekuwa ikishuhudiwa kwenye Daraja la Kimara ambako watu wamekuwa wakilazimisha kupita chini ya daraja kwa kupenya kwenye uzio na kuyaweka hatarini maisha yao.

Kutokana na kadhia hiyo, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro juzi alitoa hadhari kwa wanaotumia utaratibu huo, akisistiza adhabu kali zitatolewa dhidi yao.

Alisema alishatoa onyo siku nyingi na kulikuwapo na kundi kubwa la watu waliokuwa wanafanya hivyo lakini sasa wamebaki wakaidi wachache.

"Tutaendelea kutoa elimu na kuwaelimisha, wataelewa tu madhara yake, walikuwapo watukutu wengi, sasa wamebaki wachache, tutawafundisha kwa matukio kwa sababu hata wao wanaona kinachowakuta wanaokamatwa.

"Mtu akishakamatwa ndipo ataona kitakachomtokea, tutapambana nao tutawaelewesha mpaka watakapoelewa," alionya Kamanda Muliro.

Katika mazungumzo na Nipashe Jumapili, baadhi ya wakazi na wasafiri wa waliokutwa kwenye Stendi ya Mabasi ya Magufuli, walisema kinachosababisha watu kutumia njia ya kupenya chini ni mzunguko mkubwa uliopo wakati wa kuvuka madaraja hayo.

Mwajuma Shabani, mkazi wa Mbezi, alisema" "Daraja hili ni kubwa sana na lina mzunguko mrefu, ndiyo maana watu wanaamua kutumia njia ya mkato japo ni hatari sana kwa sababu hapo chini watu wanapita na magari yao, pikipiki zinapita, hivyo usalama ni mdogo. Kama serikali ikikaa kimya, kuna siku kutatokea vifo vya watu wengi hapa".

Ramsi Mazengo, mkazi wa Kimara alisema kinachosababisha baadhi yao kupenya chini ni kutotii sheria "kama ilivyo kawaida ya watanzania".

"Ukiangalia hili daraja jinsi lilivyo, lipo vizuri kabisa, shida wengine siyo jadi yao kufuata sheria tu, watu kama hao hawakosekani katika jamii, wakati mwingine unamwona mtu mzima na afya yake kabisa lakini anapenya chini, huo ni utovu wa nidhamu.

"Hali hii inatishia amani, watu wamegeuza kama njia yaani mtu anangalia huku na kule akiona hakuna askari, anainama anapenya kwenye wavu anakwenda ng'ambo ya pili, ingewezekana tungeleta hata askari mmoja wa doria hapa," alishauri Mazengo.

# Jela miaka mitatu kwa kuhonga hakimu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi mkoani Dodoma imewahukumu wafanyabiashara wawili, wakazi wa Kigamboni jijini Dodoma kifungo cha miaka mitatu au kulipa faini ya Sh. 500,000 baada ya kukamatwa wakiwa na Sh. 335,000 ambazo walitaka kumhonga Hakimu Frola Muhelele ili asitoe hukumu ya kifungo dhidi yao. Hukumu hiyo ilitolewa juzi kwenye mahakama hiyo mbele ya Hakimu Janet Mswereto na washtakiwa hao kutakiwa kutumikia adhabu hiyo.

Washtakiwa hao waliofikishwa mahakamani huko mwaka 2021 na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ni Erick Godluck na Haule Makrios kwa mashtaka mawili.

Mashtaka hayo ni pamoja na madai ya kushawishi na kutoa rushwa ya Sh. 500,000 na walidaiwa kuwa tayari walikuwa wameshatoa zaidi ya Sh. 300,000 ndipo mtego wa TAKUKURU ukawanasa.

Washtakiwa hao walidaiwa kutenda kosa hilo kinyume cha kifungu cha Sheria Na. 15 ambacho kinakataza kutoa rushwa ya aina yoyote.

Hadi Nipashe inaondoka mahakamani huko, washtakiwa hao walikuwa mahakamani wakisubiri kupelekwa gerezani au kulipa faini ya kutumikia adhabu hiyo.

Akifafanua kuhusu suala hilo, Mkuu wa TAKUKURU mkoani Dodoma, Sosthenes Kibwengo alisema kuwa baada ya hakimu huyo kushawishiwa kuchukua rushwa, alitoa taarifa TAKUKURU na kwamba taasisi ilifanyia kazi jinai hiyo mara moja.

Aliitaka jamii kuendelea kushirikiana na taasisi hilo ili kuhakikisha rushwa inatokomezwa kwenye maeneo mbalimbali.

Alisema lengo la TAKUKURU ni kuona rushwa inapigwa vita na watu wote na siyo kubaki kuwa jukumu la taasisi hiyo peke yake.

Alisema kitendo cha kudiriki kutaka kumpa rushwa hakimu ni kibaya kwa sababu hakimu ni mtu wa kutoa haki kwa kila mmoja.

# DC agawa vishikwambi kwa walimu kuboresha utendaji

**Na Mwandishi Wetu,** GAIRO

MKUU wa Wilaya ya Gairo, Jabiri Makame amegawa vishikwambi kwa zaidi ya walimu 700 ili viwasaidie katika utendaji wao wa kazi.

Walimu hao ni wa shule za msingi na sekondari wilayani hapa ambavyo vimetolewa na serikali ili viwasaidie kuboresha utendaji wao wa kazi.

Makame aligawa vishikwambi hivyo juzi wakati wa hafla ya kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuipatia wilaya hiyo fedha nyingi za miradi ya maendeleo katika sekta za elimu, afya, maji, umeme, barabara na utawala bora.

Akizungumza baada ya kugawa vishikwambi hivyo, Makame alisema Wilaya ya Gairo imetekeleza miradi yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 21 ukiwamo ujenzi wa madarasa 22 ya shule za sekondari yaliyogharimu Sh. milioni 440 ikiwa ni maandalizi ya kupokea wanafunzi 3,060 waliofaulu na kuchaguliwa wilayani hapa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu.

Makame aliwashukuru walimu wote kwa usimamizi wa ujenzi wa madarasa na kumtaka Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo kuwaruhusu walimu hao kutumia fedha zilizobakia katika miradi kuboresha ofisi zao na mahitaji mengine yanayowagusa walimu.

Vilevile, aliwataka wazazi kutimiza wajibu wao wa kuhakikisha watoto wao waliofaulu kujiunga na Kidato cha kwanza na wale waliotimiza umri wa kuanza darasa la awali na darasa la kwanza mwaka huu wa 2023, kupelekwa shuleni bila ya kuwapo vikwazo na visingizio vyovyote.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Gairo, Dastan Mwendi aliitaka serikali kuweka mikakati ya kuongeza idadi ya shule za sekondari za kidato cha tano na sita ili kuongeza idadi ya wanafunzi na kutekeleza Ilani ya chama hicho.

"Kuongezeka kwa shule hizi za sekondari za kidato cha tano na sita kutaleta ari kwa vijana wetu kupenda kusoma na pia kutapunguza gharama kwa wazazi wa watoto wanaochaguliwa kujiunga na kidato cha tano ambao wengi wao wamekuwa wanachaguliwa kwenda kusoma mikoa ya mbali," alifafanua Mwendi.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Gairo, Msifwaki Haule alisema halmashauri imejipanga kusimamia vyema miradi ya maendeleo kwa kuwa kwa kufanya hivyo serikali itaendelea kuleta fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo ili kuboresha maisha ya wananchi.

# Mambo 14 yaliyodumisha muungano Tanzania, China mwaka uliomalizika

## •Ziara ya Dk. Samia yawa neema mpya...

Na Mwandishi Wetu



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwa na mwenyeji wake, Rais wa China Xi Jinping, ziarani China.

CHINA ni taifa lenye historia ya kindugu na Tanzania, ikiwa na mzizi tangu zama miaka michache baada ya uhuru wa nchi kupatikana.

Aina ya uhusiano huo kiuchumi, unabeba picha zaidi hasa ilipofika mwaka 1964, Tanzania ilipoundwa kutoka Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na kuwapo mfumo wa siasa ya chama kimoja cha kisiasa, ambapo ujamaa ulishika nafasi rasmi, ikiendana na itikadi ya China.

Vivyo hivyo, katika kipindi hichi ndipo Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa miaka mitano, 1964 -1969 ulianzishwa, sifa yake kuu iligusa Tanzania kujimudu katika mambo ya misingi ya ndani kama elimu na uzalishaji wa mahitaji ya ndani.

Hapo ulijengwa mkakati wa sura ya uzalishaji kuondokana na kuuza nje malighafi hasa ya shambani, na kuingiza nchini iliyozalishwa kwa lugha "Kuacha kuzalisha tusichokitumia na kutumia tusichokizalisha" hadi "kuzalisha tunachokitumia."

Katika jitihada za Tanzania kupata marafiki wa kigeni wanaoiunga mkono hasa mwaka 1964, China ilionekana kuwa miongoni mwa marafiki wa kweli, hata katika sura ya kipekee kukashuhudiwa ukaribu wa Rais Nyerere na Rais Mao Tse Tung wa China.

Hali kadhalika sura hiyo hiyo inashuhudiwa kwa mawaziri wakuu; Chuo En Lai na Rashid Kawawa na mengi yakashuhudiwa katika hatua hiyo, ikiwamo Watanzania kuzama katika utamaduni wa China, kuvaa mashati yasiyo na kola, wakiongozwa na Mzee Kawawa.

Katika miaka mitano ya kwanza ya Mpango wa Maendeleo (1964 = 1969), kulishuhudiwa China kutoa misaada mingi ya maendeleo kutoka ndani ya mipango ya maendeeo hiyo, wakiwapo Watanzania wengi wanakwenda kusomea fani mbalimbali China na katika nafasi ya pekee, wanakumbukwa madaktari.

Awamu ya kwanza kukashuhudiwa maendeleo ya misaada mikubwa ikiwamo ujenzi wa viwanda, ukiwamo mfano wa Kiwanda cha Nguo Urafiki Dar es Salaam.

Lingine la kihistoria, katika awamu ya pili ya Mpango wa Maendeleo (1969- 1974) kulijengwa Reli ya Urafiki wa Tanzania na Zambia (TAZARA), ujenzi wa kimsaada na mradi mkubwa zaidi ulioanza mwaka 1970 na kukamilika 1975.

Ni aina ya historia ya uhusiano uliodumu hata mwaka 1976 Rais Mao Tse Tung alifariki, akiwa ameshuhudia ndoto yake na viongozi wa Tanzania na Zambia (Rais Kenneth Kaunda) ya treli TAZARA inatimia.

Uhusiano huo haujawahi kupotoka katika awamu zote tano zilizopita za uongozi wa Tanzania, kukikumbukwa, Rais Benjamin Mkapa wa wamu ya tatu, alifanikisha ujenzi wa Uwanja wa Michezo wa Mkapa, jijini Dar es Salaam, kwa msada wa China.

**CHINA VS AWAMU 6**

Wakati leo unaanza mwaka mpya 2023, ubalozi wa China nchini unatoa shukrani za dhati kwa wadau mbalimbali kwa ushirikiano wao uliowezesha utekelezaji wa majukumu ya Ubalozi kwa mwaka ulioisha .

Unasema katika mwaka huo, umefanikisha mambo mbalimbali yenye tija na manufaa kwa wananchi wa pande zote, ikipongeza mwongozo na maelekezo ya Mwanadiplomasia Mkuu wa nchi, Rais Dk Samia Suluhu Hassan, ikiwa na ushuhuda wa mambo kadhaa yaliyofanyika kidiplomasia:

Moja; Kati ya tarehe 2 na 4 ya Novemba mwaka jana, Rais Dk. Samia alifanya ziara ya kihistoria nchini China, inayotajwa kupandisha hadhi ya uhusiano wa kimkakati katika nyanja zote za nchi mbili.

Pili; Upande wa biashara na mauzo ya bidhaa za Tanzania katika soko la China, yaliongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 409 hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 605.5 (kati ya Sh. bilioni 961.150 Sh. trilioni 1.423).

Inatarajiwa katika mwaka mpya unaoanza , mauzo yataongezeka kwa asilimia 20 zaidi, sababu kuu ni Tanzania kufunguliwa soko jipya la bidhaa wakati wa ziara ya Rais Samia nchini China.

Tatu; Wakulima na wafanyabiashara wa Tanzania wanaoshughulika na zao la parachichi walifunguliwa soko jipya nchini China Novemba mwaka jana na linatarajiwa kushamiri katika soko la China mwaka unaoanza kesho.

Nne; Wavuvi wa Tanzania wamefunguliwa soko jipya kuuza mabondo ya samaki nchini China, hasa aina sangara kwa matarajio ni kuongezeka mauzo bidhaa za uvuvi mwaka huu.

Tano; Bidhaa za Tanzania zilizongezewa thamani na kuuzwa katika soko la China kupitia mtandao maarufu wa biashara JD.COM wenye watumiaji milioni 600, mnamo Mei, mwaka jana.

Sita; Watanzania walianza kufanya shughuli za usafirishaji mizigo moja kwa moja kutoka Tanzania hadi China, kwa kutumia Shirika la Ndege la Air Tanzania- mwezi Mei 2022. Matarajio ni mwaka huu baada ya China kufunguka, shughuli zitaongezeka maradufu.

Saba; Usafiri wa abiria wa ndege moja kwa moja kutoka Dar es Salaam hadi mjini Guangzhou China ulianza Julai, mwaka jana, unatarajiwa kuanzia Januari inayoanza kesho, wafanyabiashara, wanafunzi na watalii watanufaika na huduma hiyo baada ya China kufungua mipaka na kuondoa masharti ya udhibiti wa UVIKO - 19

Nane; Baada ya maelekezo ya Rais Samia, Ubalozi Mdogo wa Tanzania katika jijini la Biashara la China- Guangzhou ulifunguliwa rasmi Mei 2022 na Watanzania wameanza kupata huduma za biashara, ubalozi nao ukitumia fursa kufungua fursa masoko ya bidhaa.

Tisa; Filamu ya Tanzania Royal Tour ilionyeshwa katika Televisheni ya Hainan, China mnamo mwezi Oktoba iliyopita na kuangaliwa na watu milioni 60. Filamu hiyo imeshatafsiriwa kwa lugha ya Kichina na inashamiri katika mitandao ya kijamii ya China, ukiwamo yenye anwani "Bilibili m.bilibili.com/video/BV1jB4y1..."

Kumi; Wanafunzi wa Kitanzania wanatarajiwa kunufaika kwa kupata elimu ngazi za shahada na stashahada, baada ya kutiwa saini makubaliano mwezi huu Desemba, kati ya Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) na Taasisi ya Chongqing Vocation Institute of Engineering (CQVIE) ya China ya kuendesha mafunzo ya pamoja.

Kumi na moja; Vijana wa Kitanzania wataanza kunufaika na mafunzo ufundi, kutokana na kufunguliwa rasmi Chuo cha Ufundi cha VETA, mkoani Kagera kilichojengwa kwa msaada wa China na kuzinduliwa na Rais Dk. Samia, mnamo mwezi Oktoba, mwaka jana.

Kumi na mbili; Kuna Watanzania 122 wamefadhiliwa masomo ya elimu ya juu katika vyuo vikuu nchini China kwa fani mbalimbali. Mwaka mpya 2023, Watanzania wanatarajiwa kuendelea kupata fursa hizo za masomo, ikiwa ni sehemu ya matokeo ya ziara ya Rais Samia nchini China.

Kumi na tatu; Mwaka jana wafanyabiashara wa Tanzania wamepatiwa elimu kuhusu fursa za biashara zilizopo China, pia ushauri wa hatua za kuchukua katika kuepuka kuangukia mikononi mwa wafanyabiashara wasio waaminifu.

Kumi na nne; Katika mwaka 2022, vipindi vya elimu kwa umma vilianzishwa kuwapa wananchi ufahamu wa fursa za upatikanaji teknolojia za bei nafuu za China, kwa ajili ya uzalishaji na usindikaji malighafi zinazopatikana nchini.



Bidhaa parachichi, iliyofungua soko kubwa nchini China.
**PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU.**

# Serikali kumega hekta 33,000 za hifadhi kuwapatia wananchi

**Na Munir Shemweta,** RUVUMA

SERIKALI imetenga jumla ya hekta 33,132.24 mkoani Ruvuma kutoka maeneo ya hifadhi na shamba la NAFCO na kubakizwa kwa wananchi kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Vilevile imebainisha kuwa wananchi wote waliovamia Hifadhi ya Msitu wa Lihanje ulioko Halmashauri ya Wilaya ya Songea wanapaswa kusitisha shughuli zozote za kibinadamu kwenye maeneo ya mlimani na bondeni.

Hayo yalielezwa juzi na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula katika kikao cha Kamati ya Mawaziri Wanane wa wizara za kisekta na uongozi wa Mkoa wa Ruvuma wakati kamati hiyo ilipofanya ziara kwa ajili ya kutoa mrejesho wa uamuzi wa Baraza la Mawaziri kuhusiana na Utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi kwenye vijiji 975.

Dk. Mabula ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mawaziri Wanane alisema Mkoa wa Ruvuma unahusisha vijiji/mitaa 38 yenye migogoro ya matumizi ya ardhi ambapo uamuzi wa kamati ni kumega sehemu ya maeneo ya hifadhi kuwaachia wananchi sambamba na kusitishwa shughuli za kibindamu kwenye hifadhi.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, wakati wa tathmini kuhusu migogoro ya matumizi ya ardhi kwenye Mkoa wa Ruvuma, timu ya wataalamu ilivifikia vijiji/mitaa 38 kwenye wilaya za Mbinga, Nyasa, Tunduru, Namtumbo na Songea ambako kazi ya uandani ilihusisha na kufanya vikao na uongozi wa serikali za vijiji husika na kisha kutembelea maeneo yenye migogoro.

"Pamoja na uamuzi huu wa serikali wa kumega maeneo kwa ajili ya vijiji, mkoa unalo jukumu la kusimamia utekelezaji wa uamuzi huu kwa kusimamia utekelezaji huo kwa kushirikiana na taasisi na mamlaka zote zilizopo ndani ya mkoa na ni muhimu maeneo haya yaliyomegwa kuandaliwa mpango wa matumizi ya ardhi ili kuepuka matumizi holela," aliagiza.

Dk. Mabula, akizungumzia umauzi wa serikali kusitisha shughuli za kibinadamu kwa wananchi waliovamia Hifadhi ya Msitu wa Lihanje, alielekeza mkoa kwa kushirikiana na timu atakayoiunda, kufanya tahmini ya kina ya mahitaji halisi ya ardhi kulingana na idadi ya watu waliopo kwenye vijiji hivyo na kuahidi timu yake ya mawaziri wa wizara za kisekta kurejea tena mapema mwezi huu wa Januari kwa ajili ya kupokea taarifa na kutoa uamuzi.

"Wananchi wote waliovamia Hifadhi ya Msitu wa Lihanje kwa kuendesha shughuli za kilimo kwa maeneo ya mlimani na bondeni, wanaelekezwa kusitisha shughuli zozote za kibinadamu kwenye maeneo hayo kwa mwaka huu (mwaka uliofika ukomo jana)," aliagiza.

Msitu wa Lihanje unasimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) na ni chanzo muhimu chaa maji chenye mradi wa maji mtiririko Luyelela na Kilagano ambapo wananchi wamevamia takriban asilimia 60 ya msitu na kuendesha shughuli za kilimo.

Aliushukuru Mkoa wa Ruvuma kwa kuratibu vyema tahmini na kuwezesha kazi hiyo kufanyika kwa amani na utulivu huku akitambua mkoa huo unazo kero nyingi zinazosababishwa na mwingiliano wa matumizi ya ardhi.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana aliwataka wananchi kuwakemea wale wote wanaoharibu vyanzo vya maji na kuzitaka mamlaka zote kuanzia ngazi ya vijiji kuhakikisha zinadhibiti uvamizi wowote unaofanyika katika hifadhi za misitu na mapori ya akiba.

Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Ruvuma, Odo Mwisho alisema chama chake kinaungana na serikali kuhakikisha kinalinda maeneo yote yaliyotamkwa kuwa ni hifadhi ya asili ili kuepuka uharibifu wa mazingira na uto wa asili.

## Kaya isiyopanda miti mitano kutozwa faini

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule amesema kaya itakayobainika kutopanda miti mitano jijini Dodoma, itachukuliwa hatua ikiwamo kutozwa faini.

Hatua hiyo ni utekelezaji wa sheria ndogo na matakwa ya utoaji wa kibali cha ujenzi ambacho kinataka mtu anayepewa kibali kupanda miti mitano na asipofanya hivyo atapigwa faini na kutekeleza takwa hilo.

Akizungumza jana jijini hapa kwenye upandaji miti eneo la chanzo cha maji cha Ihumwa unaoratibiwa na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA), Senyamule alisema maofisa watendaji wa kata na vijiji wanapaswa kuchukua hatua kwenye maeneo yao kwa kaya ambazo zinakaidi kutekeleza suala hilo.

"Pamoja na vibali vya ujenzi wa makazi kutaka kila nyumba kupanda miti mitano, baadhi ya watu wamekuwa wakikaidi, hali inayochangia makazi mengi kutopandwa miti.

"Kuanzia sasa kaya au maeneo ya wazi yatakayobainika kutopandwa miti, viongozi wa eneo hilo watakuwa wa kwanza kuchukuliwa hatua," alionya. Alisema mpango wa utunzaji mazingira umetoa kipaumbele kwa Mkoa wa Dodoma kupanda miti kwenye maeneo ya vyanzo vya maji, maeneo ya wazi, maeneo ya makazi, hifadhi pamoja na urejeshaji miti kwenye maeneo ambayo miti haikustawi.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, Jabir Shekimweri alisema kuwa kwenye eneo hilo la chanzo cha maji, miti zaidi ya 2,000 itapandwa na kwamba eneo hilo lenye ekari 45 liliongezwa ukubwa kufikia ekari 350 ili kupandwa miti na kujenga bustani za wanyama.

Awali Kaimu Mkurugenzi wa DUWASA, Emmanuel Mwakabole alifafanua kuwa baada ya Makao Makuu ya Nchi kuhamishiwa Dodoma, wakazi waliongezeka na mahitaji ya maji yakaongezeka kufikia wastani wa lita milioni 133 huku uwezo uliopo ni lita milioni 67.1 kwa siku.

Alisema kuwa kutokana na uhitaji huo, walibaini chanzo kikuu cha maji Mzakwe kimefikia ukomo wa uzalishaji maji ni lita milioni 61.5 kwa siku na hivyo kuongeza vyanzo vingine vya maji ikiwamo Ihumwa, Iyumbu na vyanzo vingine vidogo. "Maana yake ni kwamba tungetegemea Mji wa Serikali upate maji kutoka Mzakwe na Mji wa Ihumwa nao ungepata maji kutoka Mzakwe, lakini vyanzo vya Ihumwa na Iyumbu vimekuwa vikiongeza kiwango cha uzalishaji maji. Ihumwa tuna visima 16 vyenye uwezo wa kuzalisha maji wastani wa lita milioni 9.1 kwa siku," alisema.



Askofu Mkuu wa Kanisa la Elim Pentekoste Tanzania (KEPT) Peter Konki akiwekwa wakfu kuwa Askofu wa Kanisa hilo kwa awamu ya nne jana pembeni mwake aliyepiga magoti ni mke wake Mary Peter. **PICHA: JALIWASON JASSON**

## Waziri Jafo ataka miradi ya mabadiliko tabianchi itunzwe

**Na Mwandishi Wetu,** MPWAPWA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo amewataka wananchi kuitunza miradi inayotekelezwa na serikali ili iwanufaishe katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Alitoa rai hiyo juzi alipozindua miradi ya visima vya maji, vitalu nyumba, josho la kuogeshea mifugo na mashine ya kukamua mafuta ya alizeti wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma, inayotekelezwa kupitia Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini (EBARR).

Akizungumza na wananchi wakati wa ziara hiyo, Dk. Jafo alisema Ofisi ya Makamu wa Rais iliamua kutenga fedha kutekeleza mradi huo kwenye maeneo mbalimbali yenye ukame ikiwamo Mpwapwa ili kutatua kero zinazotokana na athari za mabadiliko ya tabianchi. "Ndugu zangu mradi huu una thamani kubwa, tumeona wenyewe hapa kupeleka maji zaidi ya kilometa moja na kuleta umeme hapa kwenye kisima hiki ni gharama kubwa. Kwa hiyo, tuutunze mradi huu kwa maslahi mapana ya vijiji hivi," aliagiza.

Dk. Jafo pia alizitaka Kamati za Maji za Vijiji vya Nghambi na Mbugani ambako alizindua visima vya maji, kuusimamia mradi huo ili uwe endelevu na kuleta faida kwa wananchi. "Inawezekana baadaye mkaongeza na tangi lingine kutoka hili moja lililopo kulingana na maelekezo ya wataalamu, hivyo mtakuwa mmewezesha kupanua zaidi huduma hii na sisi kama Ofisi ya Makamu wa Rais tumetimiza jukumu letu la kuwasaidia wananchi kupambana na athari za mabadiiko ya tabianchi," alisema.

Vilevile, Waziri Jafo aliwapongeza viongozi wilayani Mpwapwa kwa kusimamia vyema miradi hiyo, akisisitiza kuwa itasaidia kujenga uchumi wa mtu mmoja mmoja na wilaya kwa ujumla.

Katika ziara hiyo, Dk. Jafo alizindua mradi wa josho kwenye Kijiji cha Kazania ambao utawasaidai wananchi kuogeshea mifugo na kuwaepusha na magonjwa yakiwamo yanayoenezwa na kupe.

Pia alizindua miradi ya visima vitatu vitakavyonufaisha wananchi zaidi ya 5,000 kupata maji safi.

Pia vitalu nyumba ambavyo wananchi kupitia vikundi wanalima mboga na viungo zikiwamo nyanya pamoja na mradi wa mashine ya kukamua alizeti kwenye Kijiji cha Ng'ambi ambayo hukamua tani 6.5 kwa siku na kuwasaidia wananchi hao ambao awali walifuata huduma hiyo wilayani Kongwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, Mwanahamisi Ally aliahidi kushirikiana na wananchi kuutunza mradi huo ili uwe endelevu.

Alisema atashirikiana na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kuhakikisha wanaongeza mtandao wa maji kupitia visima hivyo vilivyozinduliwa kupitia mradi wa EBARR ili huduma iwafikiwe wananchi wengi zaidi. Aliishukuru serikali kwa mradi huo, akisema kuwa maeneo mengi ya halmashauri hiyo yamekuwa na changamoto ya maji, hivyo utawanufaisha wanachi kulima mboga kupitia vitalu nyumba na kujipatia kipato.

Mbunge wa Mpwapwa, George Malima alisema tatizo la maji lililokuwa linavikabili baadhi ya vijiji kwenye wilaya hiyo, sasa limetatuliwa kupitia mradi huo.

Mkazi wa Kijiji cha Mbugani, Elena Mpanda akiishukuru serikali akisema sasa shida ya maji ni historia kwa kuwa visima hivyo vitawanufaisha tofauti na zamani walikuwa wanayafuata wilaya jirani ya Kongwa na kuyanunua kwa Sh. 1,500 kwa dumu lenye ujazo wa lita 20.

"Tunaishukuru sana serikali kwani zamani tulikuwa tunaoga mara moja kwa wiki lakini sasa hivi maji tunayo mengi tu, tunayatumia kwa shughuli mbalimbali zikiwamo kupikia na hata kujengea nyumba za kisasa," alisifu.

Katika ziara hiyo, Dk. Jafo pia alikagua maendeleo ya ujenzi wa malambo ya kuvunia maji kwenye Kijiji cha Kazania na Kiegea na kutoa maelekezo yakamilike kwa wakati.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mwaka 2023 ulete matokeo chanya katika uchumi, siasa

**LEO** ni Mwaka Mpya. Ni siku ambayo watu wote duniani wanasherehekea na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwavusha kutoka mwaka mmoja kwenda mwingine.

Katika kusherehekea siku hii, kwa waumini wa Kikristo, wamekuwa wakianzia ibada ambazo hufikia tamati saa 6:00 usiku ikiwa ni ishara ya kuanza kwa siku mpya ya mwaka mwingine. Kwa wengi ni furaha na shangwe kwa sababu wanaamini kwamba ni Mwenyezi Mungu ndiye aliyesababisha wao kufikia mwaka mwingine.

Pamoja na kundi la watu kuanzia kwenye nyumba za ibada, wengine wamekuwa wakisherehekea wakiwa katika nyumba za starehe kama vile kucheza muziki, kutumia vilevi na hata kupiga fataki na kuchoma matairi. Hii imekuwa wakati mwingine ikigharimu maisha ya watu kutokana na kulewa kupita kiasi na kuendesha vyombo vya moto kwa fujo. Matokeo yake, baadhi hupoteza maisha na wengine kupata ulemavu wa kudumu.

Ni dhahiri kwamba kusherehekea Mwaka Mpya hakuna kinachowazuia watu kufanya hivyo, bali kila kitu kinapaswa kufanyika kwa kiasi. Watu wanapaswa kusherehekea kwa utulivu, ikibidi wakiwa nyumbani na familia zao au kwenye mikusanyiko ambayo haina madhara.

Licha ya ukweli huo, Mwaka Mpya ni zaidi ya kusherehekea kuvuka kutoka mwaka mmoja kwenda mwingine. Kwa mantiki hiyo, jamii inapaswa kutumia sikukuu hii kwa kufanya tathmini ya mafanikio au changamoto walizokutana nazo mwaka uliopita na hatimaye kutafuta mbinu za kusonga mbele kwa mafanikio zaidi.

Katika ngazi ya familia kwa mfano, watu wanapaswa kufanya mapitio ya mambo waliyokuwa wameyapanga mwaka 2022 ili kuona ni wapi walipofanikiwa na wapi walishindwa kutimiza malengo yao na kujipanga kwa mwaka huu na kwa mafanikio makubwa zaidi. Maendeleo ya taifa lolote msingi wake ni familia, hivyo familia zinapaswa kujizatiti kwa kuwa na mipango thabiti ikiwamo ya malezi na ustawi wa kiuchumi.

Serikali kwa upande wake ina wajibu mkubwa wa kuangalia mipango yake kama ilivyoweka katika bajeti ya mwaka 2022/23 na mpango wa maendeleo kwa ajili ya kuwaletea wananchi wake maendeleo endelevu katika sekta za kiuchumi na kijamii kama miundombinu, uwezeshaji wananchi kiuchumi, elimu, afya, umeme na maji.


Mbali na miradi ya maendeleo, kumekuwa na mchakato wa maridhiano ya kisiasa baina ya serikali na chama tawala - Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa upande mmoja na vyama vya upinzani upande mwingine. Ni vyema mchakato huo ukaendelea na kuleta mwanga wa kuwapo kwa siasa za kistaarabu zinazozingatia umoja na mshikamano, tunu ambazo zimekuwa muhimu kwa ustawi wa taifa.

Kwa muda mrefu kumekuwapo na malalamiko kutoka kwa vyama vya upinzani kuwa demokrasia na uhuru wa kukusanyika, ikiwamo mikutano ya hadhara, vimeminywa na dola huku Jeshi la Polisi likidaiwa kutumia hoja ya usalama kuzuia mikusanyiko hiyo.

Pamoja na malalamiko hayo, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ameonyesha nia ya kumaliza chembechembe za uhasama zilizokuwa zikilalamikiwa kwa kutaka kuwe na mazungumzo kati ya vyama vya siasa na serikali. Kutokana na nia hiyo, mchakato huo unapaswa kukamilishwa ikiwamo kufanyia kazi baadhi ya mambo ambayo yamekuwa yakileta hoja kutoka kwa wapinzani na wananchi kwa ujumla.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Vijana waache kulalamika wachukue hatua

**MOJA** ya malengo ya Sera ya Vijana ya mwaka 2007 ni kuwahimiza kushiriki katika maamuzi na kupewa mitaji ya kuendesha shughuli za, ili waweze kujiletea maendeleo.

Hata hivyo, inaonekana baadhi yao hawajui sera hiyo, ambayo kimsingi inategemewa kutatua vikwazo mbalimbali vinavyowakabili na hasa katika jitihada za kuwawezesha kujitegemea kiuchumi.

Kinachosababisha hayo yote ni kutojitambua, kutopata stadi za maisha, elimu ya ujasiriamali, utegemezi unaochangia kutojishughulisha na uvivu.

Haya yanabainishwa na Mwenyekiti wa asasi ya Mpakani Tunaweza, Assi Khalifa katika mkutano wa tathmini ya mradi wa Kijana Paza Sauti uliolenga kuibua changamoto zinazowakabili vijana wa Wilaya ya Ubungo Dar es Salaam.

Katika tathmini hiyo, inaelezwa kuwa vijana wengi hawajui sera hiyo, hivyo ipo haja ya kuwasaidia, ili waijue na watambue jinsi ya kunufaika nayo, badala ya kukaa kama wako gizani.

Sera hiyo inaweza kuwasaidia kwenda sambamba na mabadiliko mbalimbali yanayotokea na hasa ya kisera na kijamii, ili waweze kuendana na ulimwengu wa sayansi na teknolojia.

Vikwazo vinavyowakabili wanaweza kuvigeuza kuwa fursa, kwa kufanya biashara mbalimbali katika maeneo wanayoishi wakajipatia kipato badala ya kukaa wakilalamika.

Ni muhimu wakatambua kuwa maendeleo yao na ustawi wao ni jambo la msingi, hivyo ipo haja wakaitambua sera yao kuifuatilia badala ya kudhani kwamba hawahusiki katika hilo.

Kama ambavyo serikali imekuwa ikisema kuwa sera hiyo itajenga msingi katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya mwaka 2020 hadi 2025, lengo likiwa ni kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati kupitia viwanda, vijana hawana budi kuwa mstari wa mbele.

Vijana wanatakiwa kuwa mstari wa mbele kuchangamkia fursa, kutokana na ukweli kwamba, wao ni nguvukazi ya taifa na ndio taifa la kesho, hivyo kuishi kama wako gizani ni tatizo ambalo wanatakiwa kuliepuka mapema.

Ikumbukwe kwamba sera inatoa dira yenye muelekeo wa kuhakikisha Tanzania inakua na vijana wenye nguvu, uwezo na ari ya kushiriki katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo, kwa ajili ya kuinua uchumi wa nchi.

Ninaamini katika hilo, serikali itahakikisha inaweka mazingira wezeshi, kwa kuandaa sera shirikishi, mikakati inayotekelezeka na mazingira ambayo ni rafiki kwa maendeleo ya vijana, kwani duniani hakuna nchi inaweza kupiga hatua ya maendeleo huku vijana wakiwa pembeni.

Hivyo, kwa kutumia mafunzo ambayo wamekuwa wakipata, ni vyema wakajikita zaidi katika kujua sera yao na wageuze vikwazo vinavyowakabili katika maeneo yao kuwa fursa za kufanya shughuli za maendeleo.

Kwa ujumla ni kwamba, huu siyo wakati wa kijana kubweteka, badala yake kuna nafasi ya kujiunga katika vikundi ili wapate mikopo ya fedha kwenye halmashauri zao, wafanye hivyo haraka iwezekanavyo.

Lakini pia ni vyema kuwambukusha kuwa utaratibu wa kupata mikopo umebadilika, kwa sasa inawezekana hata mtu mmoja akakopeshwa iwapo atakuwa ametimiza vigezo ambavyo vimewekwa na halmashauri.

Pamoja na hayo, ninaamini kuwa wakipata mikopo na kuanzisha biashara, biashara hizo zinaweza kuwa endelevu iwapo halmashauri zao zitakumbuka kuwatembelea mara kwa mara ili kujua maendeleo yao na kuwapa ushauri, ili waweze kufanikiwa zaidi.

Kwa hali ya sasa, ambayo ajira serikalini zimekuwa ngumu, wale ambao wamebahatika kufanya biashara, zinaweza kuwasaidia kumudu kuendesha maisha yao badala ya kukaa wakilalamika tu kwamba hakuna ajira.

Serikali imeweka kipaumbele kwa vijana, ndio maana kuna uwezeshwaji wao, kwa kila halmashauri kwa kutengewa fungu kwa ajili yao, hivyo ni wajibu wao kuchangamkia fursa hiyo.

Hata hivyo, tatizo ambalo limekuwa likitajwa ni kwamba wapo baadhi wanaopata mkopo wa fedha na kwenda kutumia kwa mambo mengine badala ya yale waliyoombea, na mwisho wa siku wanajikuta hawana kitu.

## SAFU

### FIKRA MBADALA

# Mwaka 2023 uwe wa matendo zaidi



Pascal Mayalla

LEO tumeuanza mwaka mpya wa 2023, hivyo naomba nianze makala hii kwa kuwatakia heri ya Mwaka Mpya. Wengi huuanza mwaka mpya kwa kuweka malengo ya mwaka kwamba mwaka huu nitafanya nini lakini katika kupanga hayo malengo, si wengi hufanya mapitio ya mwaka uliopita, walipanga kufanya nini, wametekeleza nini, wamefanikiwa nini na wamekwama nini.

Baadhi ya yale malengo ya mwaka uliopita, ambayo hayakufanikiwa, yanabebwa katika mwaka unaofuata au kama hayabebeki yafutwe na si kila mwaka unakuja na malengo mapya. Mwisho wa mwaka hufanyi mapitio, kisha unakuja na mengine na mengine. Mwisho wa siku, unakuwa huwezi kupima mafanikio yako!

Katiba ya nchi ndiyo Biblia, ndio Msahafu wa uendeshaji wa nchi yetu. Kama ilivyo Ikulu ni mahali patakatifu, Katiba ni kitabu kitakatifu kwa nchi yetu kama vilivyo vitabu vitakatifu vya Biblia Takatifu kwa Wakristo na Quran Tukufu kwa Waislamu. Hii ndiyo sheria mama ya uendeshaji wa nchi yetu.

Tofauti pekee kati ya Biblia, Msahafu na Katiba, Msahafu haubadiliki, katiba inaweza kubadilishwa, ila mabadiliko yoyote ya katiba, lazima yawe ni mabadiliko halali ya haki.

Katiba ndiyo sheria kuu kuliko zote za nchi. Viongozi wetu wakishachaguliwa, tunawaapisha kwa mujibu wa Katiba, wanaapa kuilinda na kuitetea. Ikitokea hata Rais wa nchi akakiuka Katiba, anaondolewa madarakani. Sheria yoyote ikitungwa, ikiwa ni kinyume cha katiba, inahesabika ni batili, wazungu wanasema ni "null and void". Ikitungwa sheria ambayo ni batili, kwa kwenda kinyume cha katiba ya nchi, kwa hapa kwetu ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT), kisha ubatili huo ukachomekewa ndani ya katiba yetu, inakuwa si kuibatilisha, bali ni kuinajisi Katiba.

Mwaka 2022 tuliipigia kelele najisi fulani ndani ya katiba yetu kwa kulialia na kuisema sema, hivyo tumefika hadi mwisho wa mwaka 2022 bila jambo lolote la maana kufanyika kuiondoa najisi hii. Sasa tumeingia mwaka mpya wa 2023, je, tuendelee tu kupiga kelele kwa kulialia na kusema sema tu, bila kufanya tendo lolote? Au mwaka huu tubadilike, badala ya kulia lia na kusema sema? Twende hatua moja zaidi kwa kutenda kitu? Msiwe na wasiwasi kuhusu kutenda huku, si kwa mikutano ya hadhara au kufanya maandamano bali ni kutenda kwa mujibu wa katiba, sheria, taratibu na kanuni.

Watanzania tuna fani mbalimbali. Kuna wenzetu kazi yao ni kufikiri na kupanga mikakati, hawa wanaitwa 'think tanks'. Kuna wenzetu ni viongozi, kazi yao ni kutuongoza, kuna wenzetu ni watenda kazi wao kazi yao ni kutenda kazi kwa kutumia nguvu zao. Kuna wengine tukiwamo sisi waandishi wa habari na vyombo vya habari, wa kiasili, kazi zetu kuu ni tatu, kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha, hatuna kutenda. Pia tumegawanyika makundi mawili, waandishi wa habari watangazaji na vyombo vya utangazaji ambao kazi yao ni kutangaza na kuongea tu, hakuna kutenda lolote! na waandishi wa habari wa magazeti ambao kazi yao ni kuandika tu, hakuna kutenda lolote.

Lakini ujio wa mapinduzi ya kidigitali kwenye dunia yetu na ujio wa mitandao ya kijamii, haya makundi mawili ya vyombo vya habari, yameunganishwa na mtandao wa jamii. Vyombo vya utangazaji vina kurasa zake za mitandao ya kijamii navyo sasa vinaandika. Mtu unaweza kusoma kama magazeti, navyo kwenye kurasa zake, vinatangaza na kuweka magazeti mtandao, hivyo siku hizi, kupata habari, kuangalia TV au kusoma gazeti, si lazima ukae nyumbani uwashe TV. Ukijisajili tu na mtandao fulani, unaletewa tu habari, kila inapotokea. Kwa hiyo mtu hana tena haja kusubiri taarifa ya habari saa mbili usiku, kila tukio linapotokea linatangazwa live, hivyo kufikia ule muda wa habari. Kila kilichotokea, watu wanakijua, magazeti ya kesho yake, sisi tunayasoma leo, maana kwenye kurasa zao za mitandao, kila habari inachapishwa pale pale inapotokea.

Ujio huu wa mitandao ya jamii, umemfanya sasa kila mtu kuwa mwandishi wa habari, kila mtu sasa ni mtangazaji, hali inayosababisha hata sisi ambao ni watangazaji wa kweli wa kusomea hii kazi, kujikuta hatufui dafu mbele ya watangazaji vijana wa kisasa kwenye mitandao ya jamii. Ukiwauliza vijana wa kisasa, unamjua Pasco Mayalla? atakuuliza, Pascal Mayalla ndiye nani? Utamwambia ni mtangazaji maarufu wa kipindi cha Kiti Moto, atakuuliza kiti moto ndio nini? Naomba 'link' yake nikitazame nikivutiwa, nita 'subscribe'. Unajikuta huna cha kumwambia, hivyo sisi waandishi wakongwe wa kianalojia ili tuendelee kuwapo ni lazima tubadilike na kwenda kidigitali vinginevyo tunafutika jumla!. Kwa hiyo , hivyo mwaka 2023, Pasco Mayalla nae anakuja kidigitali zaidi.

Kwa vile mimi kazi yangu ni kuandika tu na kutangaza, nikikaa chini na kuutafakari mwaka 2022, nimeandika mangapi na kutangaza mangapi na yapi yamefanyiwa kazi, nimejikuta kwa mwaka huu 2023 ili kuisaidia jamii na kulisaidia taifa, nisiishie kuandika na kutangaza tu. Ninapaswa nifanye kitu cha ziada kwa kwenda kidigitali zaidi na kufanya jambo ya kuandika na kutangaza tu.

Ndipo yale maneno ya Rais kijana wa Marekani, John F. Kennedy, aliyowaeleza Wamarekani, "usijiulize Marekani imekufanyia nini, jiulize umeifanyia nini Marekani?" Hivyo tunapouanza mwaka mpya wa 2023, kama kila mmoja wetu atajitafakari kwa kujiuliza "je ameifanyia nini Tanzania, akijikuta hajaifanyia kitu chochote cha maana huko nyuma, basi mwaka huu abadilike kwa kupanga malengo yenye mipango mkakati kwa kujiuliza je, ataifanyia nini Tanzania? Inawezekana kama kila mtu atatimiza wajibu wake kikamilifu, Mwaka huu wa 2023, tupunguze maneno, kuongea sana. Tupunguze kuandika sana. Hayo maneno tunayoongea sana, baada ya kuishia kuongea tu na kuandika, tufanye kwa vitendo, tutende. Hivyo jambo langu kuu la kwanza kwa mwaka huu 2023 ni Katiba!.

Japo kuna mambo mengi muhimu ya kuyashughulikia, kwangu kwa mwaka huu, naona muhimu kuliko yote ni la Katiba. Kwenye hili la Katiba, sasa tufanye kitu, tusiishie kuongea na kuandika tu bali tufanye kitu cha ziada. Je, tufanye nini? Ungana nami wiki ijayo, nikiianzisha safari ya Katiba!.

**Heri ya Mwaka Mpya.**

**+255 754 270403**

### MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Chifu Hangaya fanya kweli Mwaka Mpya



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

ASALAAM aleykum Wabongo wenzangu! Huu ni mwaka mpya, shukuruni kwa kuuona, licha ya maji kuita mma! Mliodhani siku zinaganda, naona mnashangaa kuona leo ni tarehe mosi ya mwaka mwingine kabisa.

Mmezungukwa na vitegemezi kila kimoja na shida yake, ingawa vyote vinazungumza lugha moja ya ada, madaftari, penseli, viatu, soksi, sare, tai, leso na begi.

Pembeni mama au baba mwenye nyumba naye anakuangalieni kwa matumaini ya kutia saini mkataba wa miezi mitatu, sita au mwaka wa pango lake, akiamini mlichokifanya Krismasi hakimhusu kwani kilikuwa kiherehere chenu.

Ila kwa kifupi nakutakieni Heri ya Mwaka mpya, hususan wale mliokomaa mjini hata baada ya kutishwa wakati fulani na jamaa fulani kwamba ukifika mwezi wa saba hamtaonekana mjini kutokana na ugumu wa maisha. Lakini pamoja na wale ambao mliambiwa wakati fulani kuwa lazima mtaishi kama mashetani, mkakomaa mpaka sasa mnaendelea kuishi kama malaika. Mungu hataniwi kabisa kwani ana kudra nyingi na tofauti kwa kila mja wake.

Haya, mwaka 2022 ndio huo tena, umekwenda na ukitangulia nao, akiwamo Malkia Elizabeth II wa Uingereza na galacha wa soka duniani, Edson Arantes do Nascimento 'Pele' wa Brazil na maskini wenzetu wakiwamo wa Ukraine. Mungu awapumzishe pema peponi.

Hakika mwaka uliopita uliendelea kuwa mgumu lakini si sana kama ilivyokuwa miaka mitatu, minne iliyopita. Tumshukuru Chifu Hangaya ambaye alikaa chini na kuona ni jinsi gani ya kutunyonyesha na kutulea na sasa tunauona mwaka mwingine.

Chifu Hangaya ameendelea kuwa mwema hasa baada ya kuomba ridhaa kwenye chama chake ya kutaka kupanga safu yake. Pamoja na kuridhiwa, akaona bora avute muda ili watu wale Noeli na Mwaka Mpya kabla ya kuwapanga kunakohusika.

Bila shaka katika wenye dhamana tayari wameshafungasha virago wakisubiri kauli ya Chifu Hangaya, ya ama kubaki au kurudi walikotoka kwa baba na mama zao na kufanya kingine cha maslahi kwao.

Si siri kwamba mwaka uliopita tulishuhudia baadhi ya viongozi wakishindwa kwenda na kasi ya Rais Samia Suluhu Hassan mpaka kushindwa kuvumilia na kuweka hadharani kuwa lazima afanye mageuzi katika safu yake ya viongozi.

Hakika, wako viongozi walioshindwa kutimiza wajibu wao wa msingi, mpaka pale waliposikia Rais Samia anakuja maeneo yao ndipo walipoamka usingizini na kujisemea hili na lile, huku changamoto za wanaowaongoza zikiendelea kutamalaki.

Kama kiongozi mkuu wa nchi aliapa kuhakikisha matatizo na kero za wananchi zinapungua kama si kuondoka, halafu anakuwa na wasaidizi wanaoshindwa kumsaidia katika hilo, atakuwa na maana gani kuendelea nao zaidi ya kuwaweka kando na kuja na wengine?

Hakika Tanzania hii yenye watu zaidi ya milioni 61 sasa, ina watu wa uhakika wa kumsaidia Rais kusaidia wananchi wake, kuondoka katika lindi la matatizo luluki yanayoendelea kujiimarisha kadri miaka inavyopindukia. Hata hivyo, siri kubwa ni kuja na Katiba Mpya ambayo itaondoa masharti ya waziri kutokana na wabunge, ili Rais apate wigo mpana wa kuteua watendaji hususan mawaziri, wasiotokana na Bunge.

Hakika huko nje ya Bunge kuna watu wenye uwezo mkubwa wa kuongoza na kusimamia mambo, isipokuwa wanakosa fursa hizo kwa kukosa sifa ya kuwa wabunge na hata wanaoteuliwa idadi yao ni ndogo, hivyo kunyima mwanya wa kuwapata hao wenye sifa.

Hata hivyo, kwa sasa nina uhakika wakati mchakato wa Katiba Mpya ukiwa njiani, Rais aangalie nani hasa wenye sifa ya kumsaidia kuongoza Watanzania waliochoshwa na ahadi hewa za kuwaondolewa changamoto zao.

Watanzania wanaona na kubaini ni nani kiongozi mwenye uwezo wa kumsaidia Chifu Hangaya kilivusha Taifa katika changamoto zilizopo zikiwamo za nishati, maji, kilimo, afya, madini na nyingine.

Kumekuwa na dhana, kwamba vijana ndio wachapakazi wanaoweza kulisaidia Taifa hili, lakini ukweli ni kwamba uongozi ni karama, sifa si kijana si mzee katika kuongoza, bali yeyote anaweza kufanya hivyo, kulingana na karama aliyonayo.

Lakini pia si kweli kwamba viongozi wazuri na wenye uwezo lazima watokane na chama tawala bali hata katika vyama vingine wapo, ndiyo sababu hili suala la waziri kutokana na ubunge, bado linaleta ukakasi kwani linatupa wigo finyu wa kupata viongozi tunaowataka.

Nakutakia Chifu Hangaya heri ya Mwaka Mpya lakini pia nikikutaka kutoangalia makunyanzi kwa kutuletea viongozi wachapakazi, wanaojiamini, wasioishi kwa kukusifia huku wakiboronga kazi unazowapa. Happy New Year kwa woteee!

**Alamsiki!**

# HABARI PICHA



Waandishi wa Habari wa vyombo mbalimbali wakimsikiliza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk.Hussein Ali Mwinyi.(hayupo pichani) akizungumza na waandishi ikiwa ni kawaida yake kila mwisho wa mwezi, mkutano huo ulifanyika katika ukumbi wa Ikulu Jijini Zanzibar. **PICHA: IKULU**



Mama Lishe katika eneo la ofisi za magazeti mtaa wa Majengo Kilimanjaro wilayani Muheza Tanga Mboni Husseni akipika chapati jana asubuhi kwa ajili ya kuwauzia wateja wake.**PICHA: STEVEN WILLIAM**



Sehemu ya washiriki wa kikao baina ya Kamati ya Mawaziri Nane wa Wizara za Kisekta na uongozi wa mkoa wa Ruvuma. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Rosemary Senyamule akipanda miti katika eneo la chanzo cha maji cha Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) kilichopo Ihumwa ikiwa ni mwanzo wa kampeni aliyoizindua ya upandaji miti kwa lengo la kuikijanisha Dodoma. Jumla ya miti 2000 imepandwa katika eneo hilo jana. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# MAISHA

JANUARI 1, 2023
Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 15

## Ifanye nyumba yako kila mtu aifurahie




Ukurasa 14

## Mkate wa mayai



## TOKA HIVI 2023


Ukurasa 13




# UREMBO WA HINA

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA







| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | J | A | Z | W | A |
| ■ | A | ■ | ■ | A | ■ |
| A | M | A | ■ | K | ■ |
| ■ | B | ■ | D | A | U |
| ■ | I | ■ | ■ | T | ■ |
| T | A | M | B | I | ■ |

## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
UDA, UGA, SANDA, PENDO, DANDIA, PAGAWA

## TOA TOFAUTI 5



## AMSHA AKILI

HAYA, TAFUTA NJIA



## WATOTO

## PAKA RANGI




## CHEKA

Mazungumzo kati ya marafiki wawili yalikua kama ifuatavyo;

Juma: Habari yako kijana?

John: Safi tu nambie,

Juma: Muda kweli naona unahangaika kumwagilia maziwa juu ya mikate, kwani ina matatizo?,

John: Nataka iwe laini kama ile ya dukani aliyonunua baba , akaniambia eti ni mikate ya maziwa.

Juma: Hapo unaharibu, ile inawekwa maziwa katika ngano na kisha inaokwa ikiwa na maziwa ndani na sio kumwagilia kama wewe.

SWALI
Tunda la fenesi kuna nini ndani yake?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Siri unayopaswa kujua mwaka 2023

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mada zetu za Maisha Ndivyo Yalivyo. Una kila sababu ya kumshukuru sana Mungu kwa kutuvusha salama kuuona mwaka huu mpya. Wapo wengi walitamani lakini haikuwezekana. Yote hayo ni ya Mungu mwenyewe.

Leo msomaji wangu tunapoukaribisha mwaka huu mpya 2023, hebu nikupe siri unazopaswa kuzijua unapoukaribisha mwaka. Siri ni mbinu, ni fumbo ukilifumbua utapata kitu cha thamani. Je, umefanya maandalizi gani. Kila kitu kinahitaji maandalizi. Ukiona wachezaji wameshinda, walifanya maandalizi.

Mungu anasema katika moja ya neno lake, "Siri ya BWANA iko kwao wamchao". Kabla hatujaingia mwaka 2023 zipo siri ambazo unapaswa kuzijua. Lazima yapo maandalizi unayopasa kuyafanya kukusaidia kule unakotaka kwenda.

Hakuna mwanadamu anayependa kuwa mtalii wa mwaka. Na mwaka ni namba.

Mtumishi mmoja wa Mungu akasema, 'hakuna mwaka mpya ila kuna mtu mpya'. Maana yake ni nini? Usipoangalia unaweza kujikuta ukiwa vile vile, mambo ni yale yale, maisha ni yale yale hakuna kilichobadilika kwenye maisha yako.

Kushinda au kushindwa kunategemeana na maandalizi uliyo nayo. Ndio maana watu wanapofunga ndoa, kabla ya kufikia kwenye ndoa, wanapitishwa kwanza kwenye darasa la ndoa. Yapo mafundisho fulani usipoyapata huwezi shinda kwani lazima upate maelekezo kwanza.

Sasa ni siri gani za maandalizi unapaswa kuzijua unapoingia mwaka huu 2023. Siri namba moja; kubadili mavazi. Huwezi kuwa na divai mpya ukaiweka kwenye kiriba kikuu kuu. Hapo lazima utafeli. Divai mpya inaendana na kiriba kipya.

Neno la Mungu linasema, Mathayo 9:17. Wala watu hawatii divai mpya katika viriba vikuukuu; na kama wakitia, vile viriba hupasuka, divai ikamwagika, na viriba vikaharibika; bali hutia divai mpya katika viriba vipya, vikahifadhika vyote".

Yapo mavazi unapaswa kuyavaa ili uwe mtu mpya na mwaka mpya huu uendane na wewe. Mwaka huu mpya hakuna mwanadamu mwenye akili timamu anayependa abakie pale pale. Mwaka unapovuka kuingia mpya watu hushangilia wakitamani kuwa wapya.

Mwaka mpya hushangiliwa na watu wote, wengine wacha Mungu, wengine wenye dhambi, kila mmoja kivyake. Watakatifu wako nyumba za Mungu za ibada na wengine wako beach wakishereheka mwaka mpya. Hii ni kwa sababu kila mmoja anatamani mwaka huu mpya apige hatua mpya.

Vipo vitu katika maisha yako, usipokubali kuviacha hautabadilika, hautauona upya. Yapo mambo fulani, mazoea fulani, kuna tabia fulani upo nazo na usipoziacha utabaki wewe yule yule. Huwezi kutarajia mambo mapya kwa tabia za zamani, haiwezekani!

Kama hutakubali kuachia baadhi ya vitu, kama hutakubali kubadilisha baadhi ya mitizamo yako, Kama hutakubali kuondoa baadshi ya vitu vinavyokuzuia, hautabadilika, hautauona mwaka huu mpya kuwa wa faida kwako. Utakuwa ni yule yule kwa sababu wewe ni yule yule.

Muombe sana Mungu mwaka huu akupe mambo mapya. Huwezi kutarajia mambo mapya kwa tabia za zamani. Kama yapo mambo mapya, basi kuna vitu katika maisha yako ukubali kuvidondosha, kuviacha.

Kuna baadhi ya tabia ukubali kuziacha, kama ni uvivu, ulevi, uzinzi, uwongo, usengenyaji, wizi, ulaghai na kadhalika. Ukichukua hatua hiyo, utaona mambo yanakuwa mapya!Utaona baraka mpya, utaiona imani mpya. Lakini ukikaa na kubakia hivyo hivyo, maana yake wewe ni yule yule utataka vitu vile vile.

Haiwezekani hata siku moja kutumia mbinu zile vile, tabia zile zile, bidii ile ile, nguvu zile zile upate matokeo mapya! Ili upate matokeo mapya lazima upate vitu vipya viingie ndani yako! Usimwambie Mungu badilisha maisha yangu, mwambie Mungu akubadilishe ili ujibadilishe kimaisha.

Mungu akikubadilisha, mambo yako yatabadilika yenyewe sawia. Maana zipo tabia zinavuta pesa, utajiri, watu wema. Hata kama hutawaomba kila mtu atakufuata kwa sababu palipo mzoga ndipo tai wanakuja wengi. Yaani unaomba Mungu, niletee watu wazuri, lakini tabia zako ni za zamani, tabia zako zinafukuza watu.

Ukipewa pesa unatapanya, Mungu atakupa nini na utabaki na nini? Unamwambia mtumishi wa Mungu niombee nipate pesa, tatizo siyo upatikanaji wa pesa, bali tatizo ni wewe. Ukibadilika pesa zinakaa, wateja watarudi kwako.

***Bila shaka umejifunza jambo hapo. Hadi wiki ijayo. Heri ya Mwaka Mpya 2023. Ujumbe 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Mwaka 2023 kuwapo mikakati kutunza mazingira

MWAKA 2022 umekwisha na leo tuko siku ya kwanza ya mwaka 2023. Yako matatizo tuliyovuka nayo na yako tuliyofanikiwa kuyamaliza ndani ya wakati husika.

Kwa uchache ambayo ni endelevu ni uharibifu wa mazingira uliochangia madhara mengi kama kutokuwa na mvua za uhakika, baridi kali, joto kali na majanga makubwa ya mafuriko, kimbunga na mengine ambayo yaligharimu maisha ya watu.

Kwa sasa sehemu kubwa ya ardhi imeharibiwa kwa udongo wenye rutuba kuzolewa kutokana na kilimo kisichozingatia kanuni za sekta. Pia kuna kuongezeka kwa kina cha bahari kiasi cha kumeza baadhi ya visiwa, ardhi ya kilimo na majisafi kwa binadamu na wanyama.

Ukame mkali umezikumba nchi zote na wahanga wakubwa ni Afrika ambako mifugo na wanyamapori wamekufa, binadamu wanahangaika kutembea umbali mrefu kutafuta huduma muhimu kama maji na chakula.

Kutokana na ukame, uhaba wa maji ulikuwa tatizo kubwa kiasi cha Dar es Salaam kuingia kwenye mgawo mkali wa maji, hali iliyoongeza gharama za maisha maradufu.

Pia kutokana na kupungua kwa kina cha maji kwenye mabwawa mengi ya kuzalishia umeme, mgawo mkali ulianza hali iliyoathiri shughuli za uzalishaji na maisha kuendelea kuwa magumu.

Vipindi vya mvua vimebadilika kiasi kwamba ni ngumu mkulima kuendelea kufuata ratiba ya kilimo kama ilivyokuwa awali. Badala yake mavuno yamekuwa kidogo na kupaisha bei ya vyakula kila mahali.

Wakati hali hiyo ikiendelea lilikuja janga la UVIKO-19 ambalo licha ya kutangazwa na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO),kuwa limekwisha bado limeendelea kusumbua baadhi ya maeneo hata nchini.

Wakati linatangazwa kwisha lilishasababisha madhara makubwa kwenye uchumi,kuna ambao maisha yaliharibika kabisa na kurudi kwenye umaskini,uchumi wa nchi ikiwamo Tanzania ulitikisika.

Wakati hilo likionekana kwisha ikatokea vita vya Russia na Ukraine ambavyo vinaendelea hadi sasa nchi ambazo zina raslimali na bidhaa muhimu kwa ustawi wa watu.

> **"Wakati hali hiyo ikiendelea lilikuja janga la UVIKO-19 ambalo licha ya kutangazwa na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO),kuwa limekwisha bado limeendelea kusumbua baadhi ya maeneo hata nchini.**

Mathalani, Ukraine ni mzalishaji mzuri wa ngano na mafuta ya alizeti na asilimia kubwa ya nchi za Afrika zilitegemea bidhaa hizo kutoka huko, kutokana na vita bei imepaa mara mbili.

Russia ni mzalishaji wa gesi na mafuta,kutokana na vikwazo vingi alivyowekewa na nchi za Magharibi, imekuwa ngumu kusafirisha bidhaa hiyo na sasa nchi hizo zinalazimika kutafuta kwingine na gharama kuongezeka maradufu.

Haya ni makubwa ambayo yanaendelea kuigharimu dunia,maisha ya watu na ustawi wao kwasababu yanagusa nyanza zote za maisha.

Tunapoanza mwaka 2023 lazima mikakati endelevu iwepo katika kulinda na kutunza mazingira yetu ili tusiangamie sote,inawezekana kabisa kupanda miti kwa wingi ili kurejesha uoto wa asili. Wananchi wafundishwe namna rahisi ya kuvuna maji ya mvua ili yatumike nyakati za shida. kwa kutumia matanki inawezekana kuhifadhi maji kwa kuyafanyia ukarabati mzuri ili yadumu muda mrefu na kuwa safi na salama.


Kipindi kigumu tulichopitia kiliwaumiza wengi ilifika wakati watu walianza kutumia maji ya dukani ambayo wengi wasingeweza kumudu,sasa kutokana na fundisho hilo serikali inaweza kuja na mango wa kusaidia wananchi kwa kuweka ruzuku kwenye baadhi ya vifaa vya kuhifadhia maji.

Au kuwezesha uchimbaji wa visima maeneo mbalimbali nchini ambavyo vitavuna maji ya mvua, ikiwa gharama ya kuchimba visina itakuwa nafuu wengi watafanikiwa kuwa navyo maana yake watakuwa na majibya kusaidia wakati wa ukame.

Nchi zilizoendelea kama Dubai wanatumia maji ya bahari yanaondolewa chumvi na kutumika,licha ya ukame mkali kwenye nchi hizo lakini hakuna siku wamekutana na mgawo wa maji,jambo ambalo tunapaswa kujifunza kwa kuwa tumejaliwa vyanzo vingi vya maji na mvua.

Ni muhimu kutambua kuwa iwapo kila mtu kwenye eneo lake hatafanya jitihada za kulinda mazingira kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho, kuna hatari kubwa inatunyemelea ambayo haitatuachia salama.







Kwa muda mrefu watu wamezoea kuona maharusi wakiwa katika mavazi rasmi kama suti na shela. Lakini sasa mambo yamebadilika, wanaweza kuvaa mitindo tofauti na wakapendeza kama ilivyo katika picha tofauti.



# MITINDO



## TOKA HIVI 2023

2022 utafikia tamati usiku wa 6:00, kuashiria kuanza mwaka mpya wa 2023.

Unapoanza mwaka mpya watu wanakuwa katika shamrashamra za aina yake ikiambatana na vyakula vitamu, burudani na uvaaji wa nguo za kila aina.

Katika suala la aina ya mavazi linachukua nafasi kubwa katika shamra shamra hizo, kuna baadhi wanatoka na nguo za kisasa zaidi na wengine wanaendelea na zile zinazotamba kwa muda wote.

Je aina gani ya nguo unazoweza kuvaa kipindi unapotaka kufurahia mwaka mpya? Hizi ni baadhi tu ya nguo zinazofaa kuvaliwa.

**VITENGE NA KHANGA**

Watu wengi wanapenda kuvaa nguo za vitenge au khanga ambazo kiasili ni vazi muhimu la kiafrika.

Unaweza kuvaa kitenge na khanga katika mitindo tofauti ambayo itakung'arisha na kuonekana wa kipekee.

Vazi hili linaambatana na mapambo mbalimbali ya kiafrika kama mikufu ya shanga, hereni, kofia na bangili.

SUTI NYEPESI

Suti nyepesi ni moja ya vazi zuri kuvaa katika kipindi cha mwaka mpya hasa kutokana na hali ya joto kutawala wakati wote.

Unaweza kuvaa aina yoyote ya suti, ili mradi uweze kutoka tofauti.

Hakikisha unapovaa vazi hili huambatanishi na mapambo mengi kwani saa pekee inatosha kukung'arisha kwenye mikono yako.

**MITINDO YA KISASA**

Kuna aina nyingi ya mitindo ya kisasa katika mavazi, lakini unatakiwa kuchagua ile yenye staha na maadili ya kiafrika zaidi.

Mavazi kama suruali za kubana, fulana, jeans na mashati ni baadhi tu unayoweza kupendekeza kuvaa katika kipindi cha mwaka mpya.

UREMBO

Na Mary Geofrey

# UREMBO WA HINA Zijue faida,hasara zake





HINA urembo unaotokana na rangi ya miti ya asili ambayo hujitokezsa mwilini baada ya kupaka.

Urembo huu ambao unaendelea kuishi kwa muda mrefu hapa nchini, umetokea katika nchi za Afrika Kaskazini na Asia Kusini.

Rangi ya hina inachorwa mwilini au kwenye nywele bila kutumia kemikali, hivyo ni salama kiafya.

Kwa hivyo ni lazima kutambua umhimu wa hina katika urembo, hasa kujua faina na hasara zake.

**Faida za Hina**

Unapopakwa kichwani, hina mbali na kutaka kubadilisha rangi ya nywele na kuwa ya dhahabu, pia inalinda ngozi ya kichwa kwa kuongeza maji na kupunguza mwonekano wa mba.

Molekuli zake zinazoendana na keratin ya nywele, hutoa uhai na kuangaza kwa nywele, na hivyo kukuruhusu kuitumia mara nyingi bila kuwa na hofu ya kuharibu nyuzi za nywele.

Kama tulivyosema hapo awali, ikiwa hina tunayotumia ni ya asili, basi asilimia 100 hakuna athari.

Rangi hii inaweza kutumika kwa kila aina ya nywele, ingawa matokeo bora hupatikana kwenye nywele nyeusi.

**Athari za Hina**

Hina ina kivuli kimoja tu, nayo ni nyekundu na hivyo aina nyingine za nywele ndefu zilizo na rangi kijivu haziwezi kuwa na matokeo mazuri.

Ukali wa rangi ya hina hudumu muda mfupi kuliko na rangi ya kemikali. Pia unapoosha hupungua ubora na hupoteza mng'aro.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Mkate wa mayai

MSIMU huu wa sikukuu unatakiwa kuwa mjuzi wa kuandaa vyakula nyumbani hasa kwa kuzingatia familia inakuwa kubwa na wageni wasiopungua.

Leo katika safu ya mapishi tunaelekezana namna ya kupika mkate wa mayai.

**Mahitaji**

Mayai manne, sukari vijiko viwili na nusu, unga wa ngano vijiko sita vya chakula, hiliki nusu kijiko cha chai (iliyosagwa) na backing powder nusu kijiko cha chai.

**Jinsi ya kupika**

Jinsi ya kupika mkate wa mayai unatakiwa kuchukua bakuli safi, weka ndani yake sukari na hiliki, kisha vunja mayai yote juu yake.

Changanya mayai, hiliki na sukari, kwa kutumia mashine mpaka sukari ivurugike na mayai yapande juu kama povu.

Paka mafuta chombo chako cha kuokea mkate na washa jiko lianze kupata moto.

Tia baking powder katika unga wako, kisha chukua mwiko na uanze kutia unga kidogo kidogo katika mchanganyiko wako wa mayai na sukari. Hakikisha unaukoroga vizuri kila utiapo unga ili kuepusha kuwa na madonge.

Mimina mchanganyiko wako katika chombo cha kuchomea mkate.

Oka mkate wako ndani ya jiko kwa muda wa kama dakika 20 kisha utoe.

Wacha mkate upoe kisha utoe na uweke kwenye sahani safi tayari kwa kuliwa.

**Vidokezo**

Unaweza kutupia zabibu kavu juu ya mchanganyiko wako kabla ya kuoka ili kuongeza ladha.

Kuhakikisha mkate wako kama umeiva vizuri, ingiza kijiti katikati ya mkate kisha kitoe. Kama ukigusa kijiti na unaona ni kikavu, basi ujue mkate wako umeiva. Kama kuna ubichi basi mkate wako bado haujaiva.

Kama mkate haujaiva baada ya kukagua rudisha mkate kwa dakika 5 nyingine kisha ukague tena

Sukari ikiwa nyingi mkate wako utanata na hautaiva vizuri.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Ifanye nyumba yako kila mtu aifurahie

## Namna ya kuweka sofa za michoro



KUNA vitu vingi vya kuchagua pale ambapo unaamua kupamba nyumba yako kwa jinsi unayotaka.
Aina na mitindo mbalimbali ya sofa ni mapambo inayopendezesha nyumba na kuonekana ya kisasa zaidi.
Kitambaa sahihi cha sofa kitakupatia matokeo mazuri hasa kutokana na rangi na michoro ya maua.

**Dondoo zifuatazo zitakusaidia kufanya uamuzi sahihi.**

1: Kitu cha kwanza ni kufikiria mazingira ya chumba ambacho unaenda kuweka sofa zako ili kuona kama zenye michoro au za rangi moja ndio zitafaa zaidi. Sofa zenye michoro zinapendeza kwenye chumba ambacho kina rangi moja.

2: Michoro mingi inaweza kutoa matokeo ya chumba kuonekana hakijatulia. Kwahivyo kama una pazia zenye michoro, zulia lenye michoro na pengine karatasi za ukutani zenye michoro nazo, kwenye chumba cha namna hii ni muhimu kuwa na sofa za rangi moja.

3: Inawezekana ukawa na vitu vingine vyenye michoro na hapohapo ukapenda kuwa na sofa zenye michoro. Inawezekana kabisa kuchanganya michoro, kwa mfano unaweza kuwa na pazia za michoro ya rangi nyeusi na nyeupe na ukaoanisha kwa kuwa na sofa za michoro ya kijivu na nyeupe.

4: Michoro mara zote inatakiwa iendane na ukubwa wa kitu. Sofa kubwa zinapendeza michoro mikubwa, wakati sofa ndogo zikipendeza na michoro midogo.

MIONGONI mwa maeneo ambayo huwa ni faraja ya kupumzisha akili baada ya shughuli nyingi ni nyumbani.

Nyumbani ndipo palipo na mkusanyiko wa maisha, kumbukumbu na upendo kwa asilimia kubwa ya watu.

Binadamu kila mmoja hujishughulisha na mambo mbalimbali lengo likiwa ni kujitafutia riziki na kuhakikisha mkono unakwenda kinywani na mambo mengine ya kifamilia yanakwenda sawa.

Pamoja na kujishughulisha huko, mwisho wa siku lazima arejee nyumbani kujipumzisha bila kujali umbali wake.

Hivyo basi, kwa vyovyote vile lazima uhakikishe nyumbani kunakuwa mahali sahihi, panapokupa furaha na panafanyika kuwa nyumbani kwelikweli.

Na katika kipindi kama hiki mwishoni mwa mwaka na mwanzoni mwa mwaka, wengi hupenda kuchukua mapumziko ya kikazi. Kwa hiyo ili kutengeneza mwanzo mzuri wa shughuli kwa mwaka unaofuata ni muhimu kuhakikisha nyumbani panafanyika pa faraja, amani na furaha.

Si tu kwa utulivu, lakini panawekwa vizuri kimazingira na kuwapo na mandhari ya kuvutia mtu kupumzika. Zipo njia mbalimbali za kufanya ambazo hazihitaji gharama kubwa ya kifedha ambazo ni rahisi na ni vitu vidogo vidogo.

Mojawapo ni mapambo, ndani ya nyumba yako unaweza kutafuta baadhi ya picha za mapambo ambayo unayapenda na ukapamba.

Tumia pia picha nzuri ziwe za kuchora au zinazoonyesha alama ya upendo au yoyote inayokumbusha enzi zile ukiwa nyumbani kwenu ulikozaliwa.

Ipe nyumba yako mwonekano na hisia inayotambulisha familia au aina ya watu wanaoishi katika nyumba husika au familia uliyowahi kuwa nayo awali.

Hakikisha mwonekano wa nyumba haufanani siku zote hususani ndani kuanzia sebuleni, vyumba vya kulala na hata nje kwenye mpangilio wa maua kwa wale wenye nafasi kubwa. Kila nyumba ina upekee wake na mahitaji tofauti kuendana na wakaaji wake.

Pia usafi ni jambo lingine la kuzingatia ambalo linapaswa kuzingatiwa katika kuweka mazingira yake kuwa ya kuvutia kukaa wakati wote.


Bila kusahau suala la mapishi, ili nyumbani au mtu ajisikie yuko nyumbani lazima kuwe kunapikwa chakula.

Kuna baadhi ya nyumba ambazo hakupikwi ni watu wa kula barabarani tu. Ili nyumba yoyote ile igeuke kuwa nyumbani ni muhimu sana kuwe na chakula kila wakati, yaani jiko linapotumika kuandaa vyakula na harufu yake nzuri inaifanya kuwa na uhai wa kuitwa nyumbani.

Hata wanaoishi katika nyumba hiyo lazima wajisikie fahari kuishi humo na pia kukumbuka na kupenda kuwapo nyumbani muda wote.



# KATUNI


HERI YA MWAKA MPYA WA 2023 WASOMAJI WOTE WA SAFU HII...
KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
SARAKASI, MISAMBA NA MISAMBASOTI IWE IMEISHIA MWAKA JANA AU SIO?
BADO TUNA MPYA ZA MWAKA MPYA 2023 NI MWENDO WA JUDO
NIANZEE?
NOELEEEE HEPI NIYUHIYAAA WOOYOOO...
HII HAPA TUNAISHI NAYO FUNGUA MWAKA
BAELEZELE MWAKA MUPYA UNAWAKAWAKAAA UNAMELEMETAA WAPI'BIEREE
UTAPATA LAANA KUBWA! UMEACHA KUNIPA HELA NIKALE NA WATOTO WANGU UMENILEWESHA ILI NIPEPESUKE MWAKA MPYA
USHAMWAGILIA MOYO UMETOSHEKA NDIO AKILI INAKUJIA KUWA UNAWATOTO!
KUMBE BAR NI KUPOTEZA PESA TU, ONA NIMEONGEA UMENIELEWA UMEKUWA NA BUSARA SANA, NAAMINI MWAKA HUU UTABADILIKA
ACHA PROPAGANDA EBU NISOGEZE BAR ILIYO KARIBU NIPATE KIFUNGUA MASIKIO NIKUELEWE
MGANGA WETU KASEMA MWAKA HUU HUTOBOI HUKUMJALI KAMA MIMI "UMEENDEKEZA BATA" KESHAKUKATA NYOTA
NA WEWE UMEKWENDAJE PEKE YAKO KAMA SIO SHOBO!
SHETANI GANI KAKUSIMAMIA UNIPOKEI MIZIGO!
"AMMA!"
MZIGO ULIUACHA MWAKA MZIMA BILA MAWASILIANO WENZIO WAMEUPOKEA
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...HATA KAMA UMEUONA MWAKA MPYA UNA NINI JIPYA...

## Korea Kaskazini yazidi kurusha makombora

**SEOUL,** KOREA KUSINI

JESHI la Korea Kusini limesema Korea ya Kaskazini imerusha makombora matatu ya masafa mafupi ya balestiki kuelekea baharini mashariki mwa peninsula ya Korea.

Jaribio hilo la hivi karibuni linakuja siku tano baada ya Korea Kaskazini kurusha ndege zisizo na rubani kwenye anga ya Korea Kusini kwa mara ya kwanza tangu 2017.

Korea Kaskazini imerusha makombora zaidi mwaka huu kuliko huko nyuma.

Marekani ilisema kurusha makombora hayo sio tishio la mara moja kwa Marekani au washirika wake.

Makombora hayo matatu ya masafa mafupi yalirushwa kutoka mwendo wa saa 08:00 kwa saa za huko (23:00 GMT) kutoka Mkoa wa Hwanghae Kaskazini, kusini mwa mji mkuu Pyongyang, walisema wakuu wa jeshi la Korea Kusini.

"Urushaji wa makombora ya balestiki ya Korea Kaskazini ni uchochezi mkubwa ambao unadhoofisha amani na utulivu kwenye Peninsula ya Korea na pia jumuiya ya kimataifa," waliongeza.

Walisema makombora hayo yaliruka takriban kilomita 350.

Jeshi la ulinzi wa pwani ya Japan hapo awali lilisema kombora moja lilikuwa limeanguka baharini. **BBC**

## Mfumo wa ulinzi anga Ukraine wazuia mashambulizi ya ndege

**KYIV,** UKRAINE

MAMLAKA ya mji mkuu wa Ukraine, Kyiv imesema mfumo wa ulinzi wa anga wa nchi hiyo umezuia mashambulizi ya ndege zisizo na rubani za Russia zilizolenga mji huo.

Mji wa Kyiv na maeneo jirani ya mashariki mwa nchi yanalengwa na makombora ya Russia mfululizo na kusababisha maisha kuwa magumu.

Wakati huo huo rais wa Ukraine, Volodymir Zelensky, ametangaza mipango ya kupanua mifumo ya ulinzi ya nchi yake.

Gavana wa kijeshi wa mkoa wa Kiev, Olexiy Kuleba, alisema mifumo ya kukinga makombora iliangusha ndege zisizo na rubani za Russia.

Viongozi wa jiji la Kiev walisema kwamba mashambulizi ya jana yaliyolenga mji huo yalishindwa kufikia malengo yake baada ya ndege tano zisizo na rubani kudunguliwa. **DW**



# Papa Benedict XVI aaga dunia

## ● Kiongozi wa kwanza katoliki kujiuzulu

**VATICAN CITY,** VATICAN

KIONGOZI wa zamani wa kanisa Katoliki duniani, Papa Benedict wa XVI ameaga dunia akiwa na umri wa miaka 95.

Makao makuu ya kanisa Katoliki Vatican, ilitangaza kifo cha Benedict na kusema alifariki jana asubuhi.

Benedict ambaye majina yake kamili ni Joseph Ratzinger alikuwa papa wa kwanza Mjerumani baada ya kipindi cha takriban miaka 500.

"Kwa majonzi makubwa, ni lazima nitangaze kwamba Benedict wa kumi na sita, papa wa zamani, aliaga dunia saa 9:34 leo asubuhi kwenye Monasteri ya Vatican, ambako amekuwa akiishi tangu alipostaafu mwaka 2013," ametangaza msemaji wa Vatican, Matteo Bruni.

Hali ya wasiwasi kuhusu afya ya Benedict ilianza Jumatano pale Papa Francis alipotangaza kuwa afya yake imedhoofika sana na kutaka watu wamuombee.

Papa Francis pia alimtembelea huyo mtangulizi wake huyo katika makazi yake.

Vatican haijakuwa ikitoa maelezo kamili kuhusu ugonjwa wa Benedict. Badala yake ilisema kuwa hali yake imezidi kudhoofika kutokana na umri wake.

**KUJIUZULU KWAKE**

Papa Benedict aliwashangaza wengi alipotangaza kujiuzulu Februari 28, 2013. Alikuwa kiongozi wa kwanza wa kanisa hilo kuwahi kuchukua hatua kama hiyo ya kustaafu katika karne nyingi.

Sababu ya kujiuzulu kwake alisema ni kutokana na umri wake na hali yake ya afya.

Hatua yake hiyo ilimsafishia njia mrithi wake kutoka Argentina Papa Francis. Tangu wakati huo, papa mstaafu Benedict alikuwa akiishi kwa faragha katika nyumba ya watawa huko Vatican.

Mwili wake utapelekwa katika mazingira matakatifu ya Kanisa Kuu la Mtakatifu Petro, kuanzia Jumatatu asubuhi ili kuruhusu waumini kutoa heshima zao za mwisho.

Japo hakuna utaratibu maalum kuhusu mazishi ya papa wastaafu, inatarajiwa kuwa atazikwa Vatican na mazishi hayo yataongozwa na Papa Francis.

Mnamo 2005, watu waliruhusiwa kuutizama mwili wa aliyekuwa mtangulizi wa Benedict, John Paul II, ambaye ndiye alikuwa papa wa mwisho kuaga dunia.

Mwili huo uliwekwa katika viwanja vya Vatican na watu milioni moja wakiwemo wakuu wa nchi mbalimbali duniani walitoa heshima za mwisho.

**KASHFA YA NGONO**

Papa Benedict alitajwa kuwa mwanatheolojia mahiri, lakini upapa wake ulikumbwa na mivutano ya ndani kwa ndani mjini Vatican na vilevile kashfa za makasisi kuwanyanyasa watoto kingono, matukio yaliyolitikisa kanisa la Katoliki ulimwenguni kote.

Alikosolewa kwa kukosa kuonyesha uongozi kuhusu hilo.

Dhuluma hizo za ngono ziligubika miezi ya mwisho wa uhai wake, baada ya ripoti ya kanisa la Ujerumani ya Januari 2022, kumshutumu moja kwa moja kwa kushindwa kuwazuia makasisi wanne waliokuwa wakiwadhulumu watoto kingono miaka ya 1980 alipokuwa askofu mkuu wa Munich.

Aliyakana madai hayo na Vatican ilitetea vikali rekodi yake ya kuwa papa wa kwanza kuomba radhi na kuelezea masikitiko yake kutokana na kashfa hizo na vilevile alikutana na wahanga wa kadhia hizo.

Alizaliwa Aprili 16, 1927 katika eneo la Marktl am Inn, jimbo la Bavaria nchini Ujerumani.

Aliteuliwa kuwa papa alipokuwa na umri wa miaka 78.

Kansela wa Ujerumani, Olaf Scholz alituma ujumbe wa Twitter akisema Papa huyo wa zamani alikuwa wa wengi.

" Alikuwa wa wengi, sio tu katika nchi hii, kiongozi maalum wa kanisa" alisema Scholz

Viongozi wengine wa Ufaransa na Italia nao wametoa rambirambi zao kufuatia kifo cha kiongozi huyo wa zamani.

Katika ujumbe wa Twitter, Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron, alisema anatoa salamu za rambi rambi kwa kumsifu kiongozi huyo wa zamani wa Kanisa Katoliki kwa kuunda ulimwengu wa kindugu zaidi.

"Benedict XVI alikuwa mtu wa imani na akili", alisema Waziri Mkuu wa Italia, Giorgia Meloni katika ujumbe wake.

Alisema papa huyo wa zamani alizungumza na mioyo na akili za watu na ataendelea kufanya hivyo. '

Waziri Mkuu wa Uingereza Rishi Sunak alisema amehuzunishwa na kifo cha Benedict XVI, ambaye alimtaja kama mwanatheolojia mkuu.

Sunak aliongeza kuwa ziara ya Benedict nchini Uingereza mwaka 2010, iliwakilisha wakati wa kihistoria kwa Wakatoliki na wasio Wakatoliki kote nchini humo. **DW**

MAKALA

# TEKNOLOJIA KIGANJANI CHUKUA TAHADHARI



Na Magabilo Masambu

LEO ni tarehe Mosi ya mwaka 2023. Ni Mwaka Mpya kabisa lakini si kwa upya wa mambo japo wengi wetu huwa tuna matumaini kwamba pengine magumu na changamoto tulizopitia mwaka uliopita hazitatukuta katika mwaka mpya.

Lakini baada ya muda tunajikuta hakuna mabadiliko yoyote. Kama ulikuwa na madeni mwaka uliopita, usitarajie kwamba yataisha tu kwa sababu umeingia mwaka mpya. Hizi ni namba tu kinachotakiwa ni kubadili na kubuni mbinu mpya za kutatua changamoto zetu.

Leo tuzungumze kidogo kuhusu teknolojia kiganjani. Profesa Rostow anaelezea ukuaji wa teknolojia katika ngazi ya juu kabisa kama kiashiria kimojawapo cha upigaji hatua ya maendeleo katika maisha ya mwanadamu, japo panaweza kuwapo tofauti kati ya ukuaji wa uchumi na maendeleo. Anaamini maendeleo ni mchakato lakini uchumi unaweza kukua ghafla.

Sasa kwenye teknolojia ya kiganjani nikimaanisha matumizi ya vifaa vya kisayansi kama simu, kompyuta na aina nyingine zozote za kisasa zenye kurahisisha mawasiliano na mambo mengine ni njia nzuri, lakini wakati wowote inaweza kuwa njia hatarishi kwa maisha yako na ya wengine. Ni kweli kwamba sasa kwa kutumia teknolojia kiganjani, tunaweza kutuma pesa, kukata hata tiketi za usafiri tukiwa nyumbani badala ya kwenda stendi. Yote hayo hayaondoi kuchukua tahadhari juu ya matumizi ya vifaa hivi.

Ni mwezi uliopita tu nikiwa na simu yangu mara nikapokea ujumbe kwa njia ya Whatsapp kutoka kwa rafiki yangu aishie nchini Kenya. Ujumbe huo ulikiwa unasema "Masambu unahitaji mkopo usiyo na riba?" Habari hiyo kwa mara ya kwanza ilikuwa habari njema sana kwangu. Nikataka kujua naupataje maana kwa kweli unaposikia taarifa nzuri zinazohusu pesa, lazima uulize haraka. Nilimwitikia nahitaji, akaniambia kuna watu nimewapata huku mtandaoni wao wanataka taarifa zako tu kwa maana ya majina kamili kisha utawapatia namba ya akaunti na jina unalotumia ili wakuwekee na unapata ndani ya masaa 24.

Swali la kwanza nikamuuliza, wewe umeshawapa hizo taarifa? Akasema ndiyo nishawatumia! Swali la pili nikamuuliza kwenye akaunti yako uliyowatumia kuna fedha? Akasema ndiyo ipo fedha kidogo nikamwambia kabla hatujamaliza mazungumzo haya, naomba uhamishe hizo fedha kwanza, akanambia sawa.

Alipokwenda kwenye akaunti yake kila akiingiza namba za siri anaambiwa amekosea. Baadaye akagundua akaunti yake haifanyi kazi, akanijulisha, nikamuuliza maswali yangu umeyaelewa akasema ndiyo. Nikamwambia siku nyingine isitoe taarifa zako binafsi na hasa zinazohusu akaunti za fedha.

Tazama alitumia simu yake ya mkononi kupoteza fedha alizokuwa nazo kwa kutamani kupata fedha nyingi ambazo hakuwa nazo. Wako wengine wanakuja na hadithi kwamba sijui mume wangu alifariki dunia alikuwa na fedha nyingi sana, hivyo wanakwambia wanataka waje katika nchi uliyopo mtumie fedha hizo pamoja. Mara wanakwambia tunaomba akaunti ya benki tukuingizie fedha tena wanataja mamilioni ya fedha. Sasa huu ni mwaka mwingine mpya usikubali kuingia matatizoni kwa kutumia silaha uliyoshika mkononi kujiangamiza.

Wale jamaa wa tuma kwenye namba hii bado wapo na siku hizi wamebadili mbinu baada ya kugundua kwamba tuma kwenye namba hii imeshagundulika. Sasa wanaweza kutumia majina ya watu mnaoheshimiana, yaani meseji inakuja anajitambulisha kwamba mimi ni fulani nipo kwenye kikao naomba unutumie pesa kwenye namba hii kisha nikitoka nitakurejeshea na wanataja watu mnaofahamiana.

Bahati mbaya sana ikitokea ukajaribu kupiga namba za huyo mtu ili kujua kama ni yeye ametumia namba nyingine, akawa hapatikani, unaweza kutuma kwa imani kwamba inawezekana kweli amepata shida. Ukijaribu kupiga namba ile inayotuma ujumbe anakwambia tuma meseji nipo kwenye kikao. Jua hilo tapeli moja limekaa sehemu linachoma nyama.

Mwaka uliopita pia kwa kutumia simu zetu hizi, baadhi ya watu walidanganywa kiasi cha kurekodi video za utupu na kuwatumia watu wasiyowafahamu kwa kuahidiwa kupewa fedha nyingi na watu wanaojitambulisha kuwa wako nje ya nchi kumbe unaweza kukuta ni wajinga fulani wapo hapo tu Buza kwa Rulenge! Ukishawatumia wanageuza kibao na kukufanya ATM kwamba mzigo tunao usipotuma fedha tunaachia mtandaoni kwa hiyo unageuka mtumwa ili kulinda hadhi yako. Inakubidi ukubali kutuma fedha kila wakati.

Mambo hayo yaliwakumba zaidi dada zetu wakati mwingine wanaofanya hivyo wanaweza kuwa hata wapenzi wao ambao tangu wanaanzisha uhusiano wanakuwa na lengo la kufanya hivyo baadaye. Kwa hiyo ni muhimu pia kuwa makini kama unaanzisha uhusiano baada ya kujiridhisha na mtu uliye naye.

Teknolojia mkononi zimesababisha ndoa nyingi pia kuvunjika au mauaji. Kameseji kametoka huko kalikotoka kakaingia asiyehusika kakaona, tafrani inaanza mpaka kiasi cha kukosana au kuuwana. Hebu fikiria simu ni yako, ulinunua mwenyewe bila kulazimishwa lakini inagharimu uhai wako.

Mambo ni mengi nikisema niseme yote hapa tunahitaji kuandika kitabu lakini itoshe kusema, mwaka mpya huu ni kuwa makini na matumizi ya hizi teknolojia. Muhimu zaidi kulinda taarifa zetu binafsi dhidi ya watu tusiowafahamu. Natambua kwamba kwa sasa hakuna aliye salama kuhusu taarifa binafsi lakini zile tunazoweza kuzizuia tusikubali kutoa kirahisi.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *'MV Mapenzi', 'Chatu Mkali' zilivyokoleza mipasho kwenye muziki wa dansi Tanzania*



Na Adam Fungamwango

MWAKA 1984 na mwaka 1985 ulikuwa na matukio mengi ya kufurahisha na kuhuzunisha kwenye muziki wa dansi nchini Tanzania.

Nikisema kufurahisha, nina maana kuwa ulikuwa na neema kwa makundi ya wanamuziki kutoka bendi moja hadi nyingine kwa maslahi manono zaidi.

Mashabiki wa bendi ambazo zimechukua wanamuziki hao waliibuka na furaha, huku wale ambao wamechukuliwa wakibaki na huzuni.

Mwaka 1984 kundi la baadhi ya wanamuziki wa DDC Mlimani Park Orchestra, 'Sikinde Ngoma ya Ukae', wakiongozwa na wapiga magitaa Joseph Mulenga ambaye alikuwa akipiga solo, Abdallah Gama, rhythm na Suleiman Mwanyiro mpiga gitaa la bass, walilipa kisogo kundi hilo lililokuwa kwenye kilele cha mafanikio na kwenda kuunganisha nguvu kwenye bendi ya Bima Lee, iliyokuwa ikimilikiwa na Shirika la Bima la Taifa (NIC).

Kitu ambacho mashabiki wengi walikuwa hawaelewi hadi leo ni kwamba kwenye kundi la wanamuziki waliotakiwa kwenda Bima, mwimbaji Hassan Rehani Bitchuka alikuwa mmojawapo, walikubaliana kila kitu, lakini alikwenda kwao mkoani Kigoma kwa mapumziko.

Bitchuka katika historia yake ya muziki hajawahi kupigia bendi ya Bima Lee lakini ilitakiwa iwe hivyo. Na angerejea mapema, leo hii historia ingekuwa inamtaka mwanamuziki huyo kuwa aliwahi kupigia bendi hiyo na hata nyimbo nyingi angekuwa ametunga na kuimba kwa kuthibitisha hilo.

Kwa mujibu wa Gama, ni kwamba mpaka wanaanza mazoezi ya nyimbo mpya, Bitchuka hakutokea. Na kwa wakati ule hakukuwa na simu za mkononi, hawakujua tatizo ni nini. Ndipo walipomfuata Shaaban Dede kwa ajili ya kuimba vipande ambacho angeimba Bitchuka kama angekwenda.

Hata hivyo, Bitchuka hakutokea lakini wachambuzi wa masuala ya muziki wanadai kuwa mwanamuziki huyo alishindwa kwenda Bima Lee baada ya kurejea toka Kigoma na kumkuta Dede amejiunga na bendi hiyo. Akaona bora abaki Sikinde kwa sababu yeye na mwanamuziki huyo sauti zao zinafanana.

Mwaka 1985, Orchestra Safari Sound baada ya mwanamuziki Freddie Ndala Kasheba kumaliza mkataba wake, mmiliki Hugo Kisima alikwenda kung'oa wanamuziki wa Sikinde.

Bitchuka safari hii hakupona, akachukuliwa na OSS pamoja na pacha mwenzake, Muhidini Maalim Gurumo, Ally Makunguru na Charles John Ngosha, wakaenda kuimarisha bendi hiyo na wakaasisi mtindo wa Ndekule. Mpango mzima wa kuwachota wanamuziki hao nguli, ulisukwa na Abel Barthazar Mgaitembo, aliyekuwa katibu wa bendi ya OSS. Wakati huo Barthazar, aliyekuwa mpiga solo na rhythm matata, alikuwa ametoka sikinde akaenda Bima Lee sambamba na kina Dede lakini hakaa sana na kujiunga na OSS.

Kitendo bila kuchelewa, Sikinde wakaenda Juwata Jazz Band na kumchukua mwanamuziki Fresh Jumbe aliyekuwa amejiunga kutoka Dar International ya Marijani Rajab. Wakati Gurumo na wenzake wanajiunga na OSS, Sikinde ilikuwa ikivuma na wimbo MV Mapenzi Namba Moja, uliotungwa na Mwarami Mohammed 'Golden Finger, aliyekuwa gwiji wa kucharaza Rhythm na Second Solo.

Kuondoka kwa Gurumo ambaye alikuwa kiongozi wa Sikinde ilionekana kuwa pigo kubwa kwa DDC Mliman Park lakini katika kujikaza kisabuni, walitunga wimbo MV Mapenzi Namba Mbili, ulioashiria kumpiga dongo Gurumo. Wimbo huo ambao kwa kiasi kikubwa uliimbwa na Fresh Jumbe na Cosmas Chidumule, ulimfananisha nahodha (Gurumo) kujitosa baharini na hatimaye kumezwa na nyangumi na papa baada ya meli kukumbwa na dhoruba.

Hebu tuanze na mashairi ya wimbo wa sehemu ya pili ya 'MV Mapenzi.'

"Kuchafuka kwa bahari siyo mwisho wa safari. Meli ilipokumbwa na dhoruba nahodha kajitosa baharini. Wale papa na nyangumi kwenye uchu wamemmeza ooh masikini.

"MV mapenzi, meli ya wapendanao, bendera inapepea safari yaendelea. Mabaharia wenye upendo wameikabili dhoruba, ushirikiano na bidii, ndiyo silaha yao ya ukweli na upendi ukitawala roho, kamwe hutaona mchafuko moyoni mwako."

Wimbo huo unamalizia na maongezi kati ya kapteni wa meli hiyo na mtu aliyekuwa kwenye chumba maalum bandarini akiongoza. Kapteni anamweleza mashwahibu yote yaliyowapata wakiwa safarini, meli ilivyokumbwa na dhoruba na mabaharia shupavu walioweza kumwaga maji nje ya meli na kuifanya kuendelea na safari. Pia anamwambia nahodha wao mkuu alikuwa mwoga kiasi kwamba aliamua kujitosa baharini, lakini imeshikwa na msaidizi na wanaendelea na safari.

Hata hivyo, Gurumo alijibu vikali dongo hilo kwa kutunga wimbo uitwao 'Chatu Mkali' akiwa Ndekule. Mashairi ya wimbo huo ni kama ifuatavyo;-

"Chatu mkali kwa nini wamuogopa, mnyama asiye kivuli hana mfupa, tena jabali apitapo hana pupa, apenda machakani mjini hakuzoea. Hutega njiani siku amekusudia, ni mwepesi kubaini adui kumfikia, usimchezee ndugu utaangamia, ukukute msukosuko ujute kuzaliwa.

"Usimchezee chatu, ooh chatu we, dongo usimtupie, utaukosa ushindi. Natoa onyo kwa yeyote anayemchezea chatu ni hatari, atakuwa asipate lolote la manufaa, na ajali imkute bila ya kutegemea, atakuja aadhirike ajute na dunia."

Hizo ni baadhi ya nyimbo chache za mipasho kwenye muziki wa dansi. Watu wakipigana vijembe, mipasho na kuzodoana, lakini uzuri ni kwamba alikuwa hatajwi mtu jina. Wenyewe na mashabiki ndio wanajua nini kinaendelea na walikuwa wakibishana mitaani na vijiweni kama ilivyo sasa ingawa wakati huo hakukuwa na majukwaa ya mitandao ya kijamii.

# HADITHI

# Harusi imevunjika-12

HAKUNA aliyeamini alichokisikia, wala aliyeamini macho yake kwa kile alichokiona. Awali kulikuwa na vigelegele, ngoma, bashasha na furaha tele kwa watu wote waliohudhuria harusi hiyo. Bwana harusi Jerry Mohamed aliliongoza kundi la ndugu, rafiki na jamaa kutoka Dar es Salaam kwenda Kibaha kwa Mathias mkoani Pwani kwa ajili ya kufunga ndoa na mwanamke Vayajo waliyekubaliana kuoana. Mabasi, magari, bajaji, bodaboda, vyote vilimiminika kwenda huko kila mmoja akiwa na furaha tele. Kilichotokea ndicho kilicholeta mkasa mzima kwenye sakata hili la aina yake. Nini kimetokea? Kwa nini? Sababu ni nini? Na baada ya hapo nini kinaendelea? Kila nakala yako ya Nipashe itakupa majibu ya kisa hiki cha kushangaza.

Na Adam Fungamwango
(0716 350534)

SI nilikwambia wewe, kubali akuchukue moja kwa moja kwa mahari ile ile ya dada yako ukakataa, haya sasa ndugu yako huyo huyo amekulisha nyama haramu, hujafanya chochote anakutuhumu, si bora angerudi na kukukuta umehamia tu huko huko tuone kama angekufuata?"

Ikabidi Zulfa naye aangue kicheko kwa maneno ya babu yake.

"Babu wewe ni mtu mzima, nakuamini, inawezekana, lakini ngoja na mimi nifanye uchunguzi wangu, kama ni kweli basi mbona dada atakuwa ananifikiria vibaya hivyo."

"Lakini yeye si alikimbia hapa kabla ya kuja kufungishwa ndoa, sasa wivu wa nini kwa mdogo wake?"

"Hapo sasa babu, ingekuwa amefunga ndoa kweli, au wameshawahi kuishi wote, lakini hata ndoa bado, katoroka, sasa leo ndiyo anamuona mzuri eeee, hehehe, amechelewa babu weeee." Akasema huku akijitingishatingisha kwa mbwembwe na mikogo kiasi cha kumvunja mbavu babu yake.

"Kwani dada yako anataka amuombe msamaha ili warudiane au vipi?"

"Najua basi, mradi wewe umeshanipa mwongozo kuwa kisa kitakuwa ni huyo aliyemkimbia mwenyewe au?"

"We unafikiri Jerry atakubali kwa aibu ile aliyompa?"

"Mhh, babu huwezi kujua, mapenzi haya, huwezi kujua mtu rohoni mwake."

"Wewe si umeishi naye miezi miwili huko Dar, alikuwa anaonekanaje? Anamtajataja au?

"Babu nikwambie tu ukweli, mimi nimekaa naye hata kumtaja tu alikuwa hamtaji. Kuna wakati mimi nilikuwa najisahau namtaja. Kwa sura tu alikuwa anaonekana kama anachukia, ingawa hata siku moja hajawahi kuniambia hapendi nikimtaja, lakini alionekana kabisa anakuwa kama hataki hivi, na mimi nikabadilika nikawa sisemi lolote kuhusu da' Vayajo."

*******************************

"Naa, mwenzako nimevumilia, lakini yamenifika hapa." Akasema huku akiuweka mkono wake wa kulia kwenye koo kuonyesha yalipomfika.

"Nini tena Vayajo, na wewe umeshaanza..."

"Siyo nimeanza. Unajua tangu nirudi huku Msangani sijamsimulia mtu yeyote kilichonikuta huko Naa."

"Kitu gani nilichokukuta, maana mama wewe umetoka hapa umetukimbia, sisi tumetwimbilika usiku mzima, tumekesha mama, he mara hatukuoni na hadi urudi hujataka kumhadithia lolote ilikuwaje na nini kilitokea."




**"Mimi nilijua tu itakuwa hivyo shoga, haiwezekani umkimbie mwanaume siku ya ndoa, halafu uende kwingine na si kwa mwanaume mwingine. Sasa imekuwaje ukarudi?"**

"Ndiyo hilo dada nilitaka nikwambie na hadi kwa nini nimerudi huku. Unajua nimevurugwa shoga yangu. Maana nimekosa mwana na maji ya moto."

"Enhee, nipe ubuyu shoga yangu."

"Mmmh! Na wewe nawe kwa ubuyu, hadi unataka ugeuke uniangalie usoni wakati nakusuka hapa."

Yalikuwa ni maongezi kati ya Vayajo na shoga yake Nasma chini ya mwembe karibu na nyumba ya kina Nasma.

Vayajo alimtembelea shoga yake ambaye alimuona amsuke, amfungefunge japo mabutu tu.

"Unajua nimekaa na siri hii naona donge tu limekaa hapa, sijakusimulia japo wewe shoga yangu, nilikuwa nakupigia simu kukuuliza mambo ya huku, lakini sijawahi hata kukwambia niko wapi." "Na mimi wala sikutaka kujua shoga yangu, ya nini mradi tu mzima basi."

"Lakini chonde chonde shoga yangu iwe siri yako. Sitaki niisikie kwa mtu yoyote hapa kijijini. Nikiisikia najua wewe. Na ushoga wetu utaisha siku hiyo hiyo."

"Nani? Mimi? Vayajo tangu tuko shule, umeshawahi kusikia siri yoyote yako nimeitoa?"

"Ndiyo maana hadi leo wewe umebaki shoga yangu na wewe ndiye nakusimulia hii kwa mara ya kwanza kwa sababu nakuamini."

"Funguka shoga funguka mtoto wa kike." Akachombeza ili Vayajo aseme kila alichotaka kukiongea yeye mwenyewe baada ya kukaa nalo moyoni kwa siku zote. "Shoga nikwambie ukweli kuwa mimi nilikwenda Dar es Salaam kwa mwanaume."

"Mimi nilijua tu itakuwa hivyo shoga, haiwezekani umkimbie mwanaume siku ya ndoa, halafu uende kwingine na si kwa mwanaume mwingine. Sasa imekuwaje ukarudi?"Akadakia Nasma.

"Ndiyo hapo sasa nilipovurugwa. Dada we. Wakati nikiwa na mahusiano na Jerry hadi nikamleta hapa nyumbani, kuna mwanaume mwingine huko huko Dar alikuwa ananifuatilia, anaitwa Jaziru.

Si unakumbuka kipindi kile nilipokuwa naenda Chang'ombe mara kwa mara kwa dada Pude, mtoto wa mama mkubwa?"

"Nakumbuka shoga."

"Basi kule ndiko nilikokutana na Jerry, halafu baadaye kuna kaka mmoja akatokea kunipenda anaitwa Jaziru. Lakini mimi Jaziru nikawa hata simuelewi hivi, akili yangu ikawa kwa Jerry na yeye nikatokea kumpenda sana hadi nikaja kumtambulisha huku.

Shoga we, kijana wa watu kumbe kaenda kwa da' Pude kachukua namba yangu mpya, akaanza kunisumbua. Nikawa kuna wakati natoroka hapa nakwenda Dar, siendi kwa Jerry nakwenda kwa Jaziru. Yule kaka naye sasa akaniambia kuwa anataka kunioa. Mimi nikamwambia kuna mtu amewahi, anataka kunioa. Hakukubali, akaanza kunishawishi oooh, muache njoo kwangu, mimi nikakataa."

"Mmmh! Vayajo, umekataa vipi wakati umemtoroka hapa mwenzako?"

"Wee Naa wee, nilikataa, ndiyo maana nilikubali hadi mipango yote ya harusi inafanyika, akawa ananiletea meseji hapa, yaani Vayajo kweli umekubali kuolewa na huyo mwanaume wakati mimi nakupenda. Nikamwambia mimi nafuata maisha, wewe huna kipato kikubwa hata cha kutunza mwanamke akaishi kwa raha. Akaniambia mwenzako sasa hivi nina mchongo, ukikubali hiyo nitakuwa milionea, nikamwambia haya tutaona. Dada we siku moja kabla ya ndoa, akanipigia simu akaniambia mambo yameshatiki nina pesa za kumwaga, nina mamilioni hapa sina hata wa kutumia naye, nakutaka wewe la azizi wangu, mwenzangu kusikia hivi nikapagawa."

"He, makubwa dada wewe ndiyo yalikuwa hayo eee."

"Shoga yangu nikamwambia hapa niko ndani, mimi bi harusi kesho naolewa. Akaniambia utajiharibia mwenyewe, mimi sasa hivi ni tajiri, nimeshapiga pesa maana nataka niishi na wewe, lengo lipo pale pale. Nikamwambia kama unataka kuishi na mimi basi niamini kama kweli una hizo pesa, weka shilingi milioni tano kwenye akaunti yangu. Mama we, akaniomba namba za akaunti. Kwani ilifika hata robo saa, kwenye ujumbe wangu wa simu ikasoma nimeingiziwa shilingi milioni saba, sikuamini, nilipagawa. Sasa hapo nilikuwa niko tayari kufanya chochote shoga. Nilikuwa na hapo tena na hiyo ndoa? Mimi napelekwa saluni hapo akili yangu haipo kabisa hapa."

"Mmmh! Shoga yangu una mambo weee."

"Mambo kidogo shoga, basi narudi akanipigia simu, nikamwambia mimi sasa hivi natembea na wapambe kwa hiyo asipige simu anaweza kuharibu dili, atume tu meseji, ndiyo akaniambia amempigia simu dada yangu Pude. Hivi unajua yeye peke yake ndiyo anajua kila kitu na yeye ndiye aliyefanya maarifa ya mimi kutoroka bila mtu kujua. Nyinyi mlikuwa mnamuona kwenye sherehe, kumbe yule kaka kampigia simu akamwambia kila kitu na yeye akapigwa laki zake tano. Pude akaja akaniuliza, nikamwambia dada mimi niko tayari kuondoka, sijali chochote kitakachotokea, pesa hizo siyo mchezo. Tukaanza kupanga mbinu sasa za kutoroka. Tutatorokaje na umati ule?"

INAENDELEA JUMAPILI



# GENEVIEVE HAPATOSHI 2023

Miss Tanzania 2010, Genevieve Mpangala, ameanza mwaka 2023 vizuri baada ya singo yake 'Pole Pole' kufanya vizuri.

Kibao hicho ambacho alikitambulisha mwishoni mwa 2022, amemshirikisha rapa Mini Centrozone.

Akizungumza na Nipashe, Meneja wa msanii huyo Abou amesema mwaka huu mrembo huyo atajikita katika muziki pekee, hivyo mashabiki wake watarajie mambo matamu.

"Kama ambavyo mashabiki wamekuwa wakimpa ushirikiano katika urembo, naomba pia kumpokea katika muziki," amesema.

Amesema video ya PolePole ambayo amemshirikisha Moni tayari inafanya vizuri kwenye majukwaa ya muziki.

# CHRISTINA TOSSY AFUNGA NA 'NDOA'



MWIMBAJI anayekuja kwa kasi kwenye muziki wa Injili, Christina Tossy, ameawaomba wanandoa kuanza mwaka 2023 kwa kumtukuza Mungu.

Akizungumza na BT jana, Tossy, amesema amemaliza mwaka 2022 kwa kuachia kibao chake 'Ndoa' ambacho tayari amepata mrejesho chanya kutoka sehemu mbalimbali nchini.

"Huu ni wimbo wangu wa mwisho kwa mwaka 2022, namshukuru Mungu umewabariki wengi, unaelezea upendo na kuponya ndoa nyingi, tayari upo kwenye chaneli yangu ya YouTube," amesema Tossy ambaye mbali na kuwa mwimbaji ni mtunzi na mpigaji ala za muziki.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA

### FERNANDEZ AITAKA CHELSEA
KIUNGO wa kati wa Benfica na Argentina, Enzo Fernandez mwenye umri wa miaka 21 amekubali kuhamia Chelsea. ***(Metro)***

### BENFICA YAWEKA NGUMU
KLABU ya Benfica imesema ripoti iliyotolewa wako tayari kumuuza, Enzo Fernandez ambaye ni mshindi wa Kombe la Dunia wakati wa dirisha la Januari ni "uongo kabisa".***(Evening Standard)***

### MAC ALLISTER SOKONI
IKIWA uhamisho wa Enzo Fernandez hautatimia, mpango wao wa dharura wa Chelsea utakuwa ni kumsajili kiungo wa kati wa Brighton na Timu ya Taifa ya Argentina, Alexis Mac Allister, mwenye umri wa miaka 24. ***(The Times)***

### MADRID : KARIBU BELLINGHAM
REAL Madrid iko tayari kutumia zaidi ya euro milioni 100 kumsajili kiungo wa kati wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jude Bellingham, mwenye umri wa miaka 19, ambaye pia analengwa na Liverpool. ***(ESPN)***

### PERRONE ANUKIA NEWCASTLE
KLABU ya Newcastle United imekuwa ikihusishwa na kiungo wa kati wa Velez Sarsfield mwenye umri wa miaka 19, Maximo Perrone, lakini Manchester City wanaweza kuwashinda kwenye saini yake. ***(Team Talk)***

### JORGINHO KURUDI NAPOLI
MCHEZAJI Jorginho mwenye umri wa miaka 31 anataka kurejea Napoli mkataba wake na Chelsea utakapomalizika, lakini Barcelona na Newcastle pia wanamtaka kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Italia. ***(La Repubblica)***

### JIMENEZ NJIA NYEUPE
RAUL Jimenez mwenye umri wa miaka 31 huenda akaruhusiwa kuondoka Wolves katika dirisha dogo iwapo klabu hiyo itafanikiwa kusajili mshambuliaji mwingine. ***(Daily Mail)***

### PEDRAZA ATAJWA LEEDS
KLABU ya Leeds United sasa ndio timu pekee inayomsaka beki wa kushoto wa Villarreal, Alfonso Pedraza, ambaye ana umri wa miaka 26. ***(Team Talk)***

### DEULOFEU ANUKIA VILLA
ASTON Villa inavutiwa na mshambuliaji wa zamani wa Everton na Watford, Gerard Deulofeu mwenye umri wa miaka 28, ambaye kwa sasa anaichezea Udinese. ***(90 min)***

### GIL KUREJEA SPURS
WINGA wa Tottenham Hotspur, Bryan Gil mwenye umri wa miaka 21 anataka kurejea Valencia Januari hii. ***(Deporte Valenciano)***

### GYOKERES HAENDI KOKOTE
NYOTA analeyengwa na Wolverhampton Wanderers, Viktor Gyokeres, mwenye umri wa miaka 24 hataenda popote katika dirisha la uhamisho la Januari, amesema bosi wa mshambuliaji huyo wa Coventry City, Mark Robins. ***(Birmingham Live)***

### MOFFI KUTUA SOUTHAMPTON
KLABU ya Southampton imeonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji wa Lorient na Timu ya Taifa ya Nigeria, Terem Moffi, mwenye umri wa miaka 23 katika dirisha dogo la Januari. ***(Southern Daily Echo)***




# RONALDO AJIUNGA RASMI NA AL NASSR YA SAUDIA

Sasa Mreno huyo ameweka rekodi mpya ya kulipwa mshahara mkubwa...

**RIYADH, Saudi Arabia**

CRISTIANO Ronaldo amejiunga na klabu ya Al Nassr ya Saudi Arabia kwa mkataba utakaodumu hadi mwaka 2025.

Nahodha huyo wa Timu ya Taifa ya Ureno ni mchezaji huru baada ya kuondoka Manchester United baada ya mahojiano yenye utata ambapo aliikosoa klabu hiyo.

Ronaldo ameripotiwa atapokea mshahara mkubwa zaidi katika historia ambao ni pauni milioni 177 kwa mwaka.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37 amesema "natamani kupata uzoefu wa ligi mpya ya soka katika nchi tofauti".

Ronaldo aliongeza: "Nina bahati nimeshinda kila kitu nilichodhamiria kushinda katika soka la Ulaya na ninahisi sasa huu ni wakati mwafaka wa kubadilishana uzoefu wangu Asia."

Al Nassr - mabingwa mara tisa wa Ligi Kuu Saudi Arabia (Pro League) - walielezea usajili huo kama "historia inayoundwa".

Klabu hiyo ilisema "itahamasisha ligi yetu, taifa na vizazi vijavyo, wavulana na wasichana kuwa bora zaidi ".

Katika majira ya joto, Ronaldo alikataa mkataba wa pauni milioni 305 kujiunga na timu nyingine ya Saudi - Al Hilal - kwa sababu alikuwa ameridhika kubakia United.

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI

LENS
VERSUS
PARIS ST GERMAIN

1 | 3.10
X | 3.34
2 | 2.21

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# BENZEMA ATABIRIWA MAKUBWA 2023




**MADRID, Hispania**

KOCHA Mkuu wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, alitoa onyo kuhusu, Karim Benzema, kuwa bora zaidi mwaka 2023 baada ya mshindi huyo wa tuzo ya Ballon d'Or kufunga mabao mawili katika ushindi wa magoli 2-0 dhidi ya Real Valladolid, hapo juzi.

Benzema alikosa Fainali za Kombe la Dunia 2022 huku Ufaransa ikimaliza katika nafasi ya pili kutokana na jeraha alilopata usiku wa kuamkia michuano hiyo.

Na baada ya michuano hiyo, alitangaza kustaafu kucheza soka la kimataifa.

Fowadi huyo mwenye umri wa miaka 35 aliondoa masikitiko hayo katika mchezo wa kwanza wa Madrid tangu kurejea kwa LaLiga, akifunga penalti dakika ya 83 kabla ya kuongeza dakika sita baadaye.

"Namwona Benzema amehamasika sana, na nadhani utaona tofauti kuanzia 2023," alisema Ancelotti akiambia DAZN.

Katika mwaka wa kalenda wa 2022, Benzema amehusika katika mabao mengi katika mashindano yote kuliko mchezaji mwingine yeyote wa LaLiga, akiwa na 40.

Benzema alifunga mabao 44 katika mechi 46 alizoichezea Los Blancos msimu uliopita lakini amekuwa na jeraha lililotatizwa msimu huu, akifunga mara nane katika mechi 13.

Kuhusu uchezaji wa timu yake, Ancelotti aliiambia LaLigaTV: "Kuna habari nyingi nzuri kutoka kwa mchezo huu.

# Fernandez akubali kujiunga Chelsea

**LONDON, England**

MCHEZAJI wa Benfica, Enzo Fernandez, amekubali kujiunga na Chelsea wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari, kwa mujibu wa Metro.


Nyota huyo aliichezea Argentina na kutwaa ubingwa wa Kombe la Dunia, hivyo kusababisha uvumi wa uhamisho.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 alituzwa kwa juhudi zake na kutajwa kuwa Mchezaji Chipukizi wa mashindano hayo.

Fernandez alijiunga na Benfica akitokea River Plate mwaka jana, akisaini mkataba wa miaka mitano ambao unamalizika 2027.

Fabrizio Romano ameripoti The Blues wameanzisha mazungumzo na klabu hiyo ya Ureno kuhusu uhamisho, huku akitajwa kugharimu pauni milioni 105 kutokana na kipengele cha kuachiwa.

Benfica wameonyesha nia ndogo ya kumuuza Fernandez na Chelsea tayari wana mpango wa kumsaidia endapo hatua hiyo haitatokea.



CHEZA USHINDE KASINO

# MLANDEGE YAFIKIRIA MAZURI MAPINDUZI CUP IKIANZA LEO

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR.**

PAZIA la mashindano ya Kombe la Mapinduzi kwa mwaka 2023 linatarajiwa kufunguliwa rasmi leo kwa Maafande wa KVZ kuvaana na Mlandege kwenye Uwanja wa Amaan, visiwani hapa.

Mechi hiyo ya ufunguzi itacheza kuanzia 10:15 jioni na baadaye itafuatiwa na mchezo kati ya Malindi dhidi ya Jamhuri kutoka Pemba.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Mlandege, Abdallah Mohamed 'Bares' alisema timu yake imejiandaa vyema kuhakikisha wanaanza vizuri mashindano hayo kwa kupata ushindi katika mchezo huo wa ufunguzi.

Bares alisema lengo lao ni kuhakikisha kwa mwaka huu timu hiyo inatinga hatua ya fainali na kuiondosha aibu Zanzibar ya timu zake kuwa washiriki na si washindani katika mashindano hayo.

Kocha huyo alisema anafahamu ugumu wa michuano hiyo kutokana na kushirikisha timu kubwa zenye uzoefu kutoka nje ya Zanzibar kama Simba, Yanga na Azam, hivyo wamejiandaa kupambana ili kufikia malengo yao.

"Nawajua vizuri KVZ, kwa sababu nimeshakutana nao mara kadhaa katika michezo ya Ligi Kuu Zanzibar, hivyo mechi hiyo tutegemee itakuwa wa upinzani mkubwa," alisema Bares.

Naye Kocha Msaidizi wa KVZ, Ali Khalid, alisema timu yake imejiwekea malengo makubwa katika mashindano hayo na wanaamini watafikia kwa sababu wachezaji wao wamejipanga.

"Tunatarajia kushinda mechi zote na kufanikisha malengo yetu, tunataka kufanya vizuri zaidi mwaka huu," Khalid alisema.

Mashindano hayo yataendelea tena kesho kwa Aigle Noir kutoka Burundi kuvaana na Chipukizi wakati KMKM yenyewe itawakaribisha Singida Big Stars, mechi zote zitachewa kwenye Uwanja wa Amaan.



Kocha, Abdallah Mohamed 'Bares',

## Simba SC yaweka rekodi 3

INATOKA UK. 24

ka katika mabao manne kwenye mechi hiyo, akifunga matatu na kutoa pasi ya goli moja, lakini aliwaahidi wanachama na mashabiki wa Simba bado wanaendelea kufanya usajili.

"Hatujamaliza usajili, kama huu mmoja tu umekuwa na mafanikio makubwa namna hii kwa mechi moja tu, hao wengine wanaokuja sijui balaa litakuwaje," alitamba Ahmed.

Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, alisema kuwepo kwa kocha wa viungo ndani ya timu hiyo ni siri kubwa ya mabadiliko ya viwango vya wachezaji wake.

Mgunda amewapongeza wachezaji kwa kuonyesha kiwango safi katika ushindi huo mnono waliopata dhidi ya Prisons ambayo huwapa changamoto kila wanapokutana.

Kocha huyo alisema timu yake imekuwa na mabadiliko makubwa tofauti na awali kwa sababu ya ushirikiano wa benchi hilo na kocha wa viungo katika kuhakikisha wachezaji wanakuwa na viwango vizuri.

"Prisons walikuwa na malengo ya kupambania Sh. milioni 30 walizoahidiwa na sisi (Simba), tulitaka kutimiza malengo yetu ya kusaka alama tatu muhimu katika mchezo huo. Kiwango cha nyota mpya (Ntibazonkiza) ni kizuri na uzoefu wake utasaidia kikosi, tunaimani uzoefu wake utatusaidia katika michezo yetu ya ndani na kimataifa ndio maana tulimsajili kwa kipindi kifupi ameonyesha kitu," aliongeza Mgunda.

Kikosi cha Simba jijini kesho kuelekea Zanzibar katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi ambapo Simba watacheza mechi yao ya kwanza dhidi ya Mlandege keshokutwa kwenye Uwanja wa Amaan.

## Yanga yaendeleza furaha ikiingia mwaka 2023

INATOKA UK. 24

wachezaji wa Yanga kupunguza kasi ya mashambulizi, hivyo kwa muda mrefu mpira kuchezwa katikati ya uwanja, kuwafanya mabeki wa Mtibwa Sugar waliokuwa wakiongozwa na Vedastus Mwihambi, Geofrey Kuseke na viungo, James Kotei na Omari Sultan, kupumua kidogo.

Kipindi cha pili Mtibwa Sugar ilionekana kubadilika na kuanza kupeleka mashambulizi langoni mwa Yanga, ingawa hayakuwa na hatari.

Aziz Ki ndiye alionekana hatari zaidi kwenye lango la wenyeji kwani alipiga mashuti mengi ambayo yalikuwa yakitoka juu ya lango au kupanguliwa na Shekimweli, huku Mwihambi akimdhibiti kinara wa mabao katika ligi hiyo, Fiston Mayele, asifurukute na 'kutetema', kazi ambayo ilifanikiwa.

Kama wangekuwa makini, Bakari Mwamnyeto na Mayele wangeweza kufunga mabao kwa nyakati tofauti baada ya kumiminiwa krosi na Aziz Ki aliyekuwa kwenye kiwango cha hali ya juu jana, lakini walipiga vichwa fyongo, mpira ukatoka nje.

Timu zote zilifanya mabadiliko, Yanga ikiwatoa Aziz Ki, Moloko na Farid Mussa, ikawaingiza Gael Bigirimana, Dickosn Ambundo na David Brayson, wenyeji wakiwatoa Sultan na Ismail Mhesa, wakiwaingiza dimbani Mkele Joseph na Onesmo Mayaya, lakini hayakubalisha matokeo.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 01/01/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 4350 | Arman Gohar Sirjan vs Esteghlal Khuzestan | 3.30 | 2.75 | 2.49 |
| 15:00 | 5766 | Blackburn vs Cardiff | 2.30 | 3.23 | 2.98 |
| 15:50 | 3216 | Al-Thaid vs Gulf FC | 2.07 | 3.85 | 3.05 |
| 15:50 | 3295 | Masafi vs Dubba Al-Husun | 5.80 | 4.70 | 1.45 |
| 15:50 | 4125 | Masfoot Sports Club vs Ahli Al-Fujirah | 2.02 | 4.10 | 3.05 |
| 16:00 | 4927 | Coastal Union vs Namungo | 2.75 | 2.85 | 2.85 |
| 16:30 | 5932 | USM Alger vs RC Arbaa | 1.39 | 4.10 | 7.22 |
| 17:00 | 1032 | Angers vs Lorient | 2.73 | 3.28 | 2.47 |
| 17:00 | 1147 | Nantes vs AJ Auxerre | 1.93 | 3.37 | 3.82 |
| 17:00 | 1941 | Toulouse vs AC Ajaccio | 2.02 | 3.28 | 3.63 |
| 17:00 | 2757 | Monaco vs Brest | 1.45 | 4.59 | 5.99 |
| 17:00 | 3333 | Tottenham vs Aston Villa | 1.63 | 3.90 | 4.74 |
| 18:00 | 1070 | Colchester vs Swindon Town | 3.06 | 3.31 | 2.22 |
| 18:00 | 1181 | Huddersfield vs Luton Town | 2.83 | 3.18 | 2.42 |
| 18:00 | 1455 | Morecambe vs Burton | 3.02 | 3.42 | 2.19 |
| 18:00 | 1648 | Halifax vs Altrincham | 2.33 | 3.31 | 2.82 |
| 18:00 | 1733 | Portsmouth vs Charlton | 1.98 | 3.41 | 3.56 |
| 18:00 | 1752 | Chesterfield vs Scunthorpe | 1.30 | 5.30 | 8.05 |
| 18:00 | 1785 | Grimsby vs Stockport | 3.42 | 3.42 | 2.02 |
| 18:00 | 2163 | Plymouth vs MK Dons | 1.84 | 3.56 | 3.91 |
| 18:00 | 2193 | Forest Green vs Port Vale | 3.22 | 3.37 | 2.11 |
| 18:00 | 2307 | Woking vs Aldershot | 1.54 | 4.03 | 5.31 |
| 18:00 | 3054 | Maidenhead U vs Wealdstone | 2.27 | 3.32 | 2.92 |
| 18:00 | 3367 | Bristol Rovers vs Cheltenham | 1.88 | 3.51 | 3.81 |
| 18:00 | 3723 | Oxford Utd vs Exeter | 1.99 | 3.46 | 3.46 |
| 18:00 | 3827 | Hartlepool vs Harrogate | 2.47 | 3.26 | 2.72 |
| 18:00 | 3861 | Oldham vs Notts County | 6.50 | 4.63 | 1.40 |
| 18:00 | 3871 | Chester vs Telford | 1.55 | 3.98 | 4.86 |
| 18:00 | 4134 | Walsall vs Mansfield | 2.43 | 3.26 | 2.77 |
| 18:00 | 4171 | Bromley vs Southend | 2.71 | 3.30 | 2.42 |
| 18:00 | 4453 | Eastleigh vs Dorking Wanderers | 1.86 | 3.76 | 3.56 |
| 18:00 | 4821 | Blackpool vs Sunderland | 2.87 | 3.22 | 2.38 |
| 18:00 | 4951 | Sutton United vs AFC Wimbledon | 2.05 | 3.12 | 3.67 |
| 18:00 | 5215 | Kings Lynn vs Boston Utd | 1.55 | 4.00 | 4.88 |
| 18:00 | 5251 | Doncaster vs Carlisle | 2.52 | 3.26 | 2.66 |
| 18:00 | 5284 | Gloucester City vs Leamington | 2.15 | 3.25 | 3.05 |
| 18:00 | 5315 | Crewe vs Tranmere | 2.92 | 3.27 | 2.32 |
| 18:00 | 5369 | Millwall vs Rotherham | 1.60 | 3.73 | 5.37 |
| 18:00 | 5530 | Peterborough vs Wycombe | 1.92 | 3.46 | 3.71 |
| 18:00 | 5641 | Coventry vs Bristol City | 2.02 | 3.42 | 3.42 |
| 18:00 | 5718 | Yeovil vs Torquay | 2.25 | 3.30 | 2.96 |
| 18:00 | 5738 | Shrewsbury vs Fleetwood Town | 2.08 | 3.26 | 3.41 |
| 18:00 | 5947 | Bradford City vs Salford City | 1.99 | 3.37 | 3.57 |
| 18:00 | 5998 | Welling vs Tonbridge Angels | 2.30 | 3.36 | 2.73 |
| 19:00 | 1871 | Lyon vs Clermont Foot | 1.38 | 4.86 | 6.94 |
| 19:30 | 2264 | Nottingham vs Chelsea | 4.95 | 3.76 | 1.63 |
| 20:00 | 2809 | Hapoel Hadera vs Maccabi Bney Reine | 2.40 | 3.00 | 2.86 |
| 21:30 | 4814 | Maccabi Haifa vs Hapoel Beer Sheva | 1.65 | 3.85 | 4.29 |
| 22:45 | 5383 | Lens vs Paris St Germain | 3.10 | 3.34 | 2.21 |
| 23:00 | 1332 | Cavaliers FC vs Tivoli Gardens | 1.92 | 3.26 | 3.69 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumapili Januari 1, 2023
Nipashe



**Benzema atabiriwa makubwa 2023**

UKURASA 22



Winga wa Yanga, Tuisila Kisinda (kulia), akijiandaa kumtoka kiungo mkabaji wa Mtibwa Sugar, James Kotei, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Manungu, Turiani mkoani Morogoro. Yanga ilishinda ba0 1-0.**PICHA: MTANDAO**

# Yanga yaendeleza furaha ikiingia 2023

## Yaichapa Mtibwa Sugar na kujiimarisha kileleni katika msimamo wa...

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa kimataifa kutoka Burkina Faso, Stephane Aziz Ki, alifunga bao pekee akiiongoza Yanga kupata ushindi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mtibwa Sugar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Manungu, Turiani mkoani Morogoro jana.

Bao hilo si tu limeifanya Yanga kuendelea kuongoza Ligi Kuu Tanzania Bara na kurudisha pengo la pointi sita dhidi ya Simba inayoshikilia nafasi ya pili, bali pia limeifanya kumaliza mwaka 2022 kwa ushindi na pointi zake 50 kibindoni.

Simba iliyoko katika nafasi ya pili ina pointi 44 wakati Mtibwa Sugar imesalia nafasi ya nane ikiwa na pointi 24.

Aziz Ki alipatia Yanga bao hilo dakika ya 26 kwa faulo ambayo ilionekana kama haina hatari yoyote, lakini mpira ukajaa ndani ya wavu.

**Baada ya Kibwana Shomari kuchezea madhambi, mfungaji alikwenda kupiga faulo ambayo iliupita ukuta wa wachezaji wa Mtibwa Sugar na ukionekana kama unakwenda kwenye mikono ya kipa chipukizi, Razack Shekimweli, lakini ul imgonga na kujaa wavuni.**

Yanga ilianza mechi hiyo kwa kasi, ikilishambulia lango la wenyeji kama nyuki, na dakika ya tatu, krosi ya Tuisila Kisinda kutoka kwenye wingi ya kushoto nusura izae bao, ilipokwenda kutua katika mguu wa Aziz Ki aliyepiga shuti kali lililopaa juu ya lango.

Mashambulizi mengi ya Yanga yalikuwa yakipitia kwa mawinga wake kwenye mbio, Kisinda na upande wa kushoto na Jesus Moloko, anayecheza kulia ambaye waliwapa wakati mgumu mabeki, David Kameta 'Duchu' na Issa Rashid 'Baba Ubaya' ambao walilazimika kufanya kazi ya ziada kuwazuia.

Angalau kuingia kwa bao kuliwafanya

INAENDELEA UK . 23

# Simba SC yaweka rekodi 3 Ligi Bara

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

USHINDI wa mabao 7-1 ilioupata juzi dhidi ya Prisons kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam umeifanya Simba kuweka rekodi tatu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiwamo kuvunja rekodi yake yenyewe ya kufunga mabao mengi katika mchezo mmoja msimu huu.

Mabao matatu ya straika, John Bocco na Saido Ntibazonkiza, yameifanya Simba kuwa timu ya kwanza kufunga 'hat-trick' mbili kwenye mechi moja.

Inakuwa ni 'hat-trick' ya pili kwa Bocco msimu huu, ambapo ya kwanza aliipata Novemba 19, mwaka jana katika mechi dhidi ya Ruvu Shooting, akiiongoza timu yake kushinda mabao 4-0 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Rekodi ya pili ni kuwa ndiyo timu yenye 'hat-trick' nyingi, ambapo mpaka sasa inazo tatu, mbili zikipigwa na Bocco na nyingine ikiwekwa na Ntibazonkiza aliyekuwa akicheza mechi yake ya kwanza msimu huu na kikosi cha Simba, akiwa amesajiliwa kipindi cha dirisha dogo akitokea Geita Gold FC.

Mpaka sasa kuna 'hat-trick' nne katika Ligi Kuu, ambapo moja ikipigwa na Fiston Mayele wa Yanga, akifanya hivyo kwenye mechi dhidi ya Singida Big Stars, timu yake ikishinda mabao 4-1.

Simba pia imeweka rekodi nyingine ya kufunga mabao mengi zaidi kwenye Ligi Kuu kwa kufunga idadi hiyo ya mabao, ikivunja rekodi yake ya mabao 5-0 ambayo iliiweka Oktoba 30, mwaka jana ilipoichapa Mtibwa Sugar na Desemba 18, mwaka jana ilipopata idadi hiyo ya mabao dhidi ya Geita Gold.

"Simba tunaamini katika mbinu, mikakati na ubora, tulisema hata kama wangewaahidi dunia nzima, lakini kama hawana ubora wasingeweza kufanya kitu, tumewafunga, tumewanyanyasa na tumewapigia mpira mkubwa," alisema Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally.

Alisema usajili wa Ntibazonikiza umeanza kulipa kwa sababu amehusi-

INAENDELEA UK . 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >